SUPA JACKPOT
TZS.1,077,433,324
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**Rais** Samia anunua mabao Simba, Yanga mechi za CAF

UKURASA 24




UKURASA 11

Nipashe
Jumatano Februari 15, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581222
www.ippmedia.com
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



Rais Samia Suluhu Hassan akishuhudia Mkurugenzi wa Shirika la Umeme (TANESCO), Maharage Chande (wa pili kulia) na Mwanasheria wa Shirika hilo, Zaharani Kisilwa (kulia), wakitia saini mikataba mbalimbali ya Gridi Imara na makandarasi Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Samia acharuka fitina za tenda

• **Azitaja** PCCB, PPRA kutumika kufanikisha 'mchongo'...

*Endelea ukurasa 2*

## Asakwa kashfa ya kubaka, kumuua mke wa M/kiti

UKURASA 7

## ...watendaji wa kata nao wanyooshewa kidole kwa uonevu

UKURASA 5

REACH A WIDER AUDIENCE THIS Valentine SEASON
AT AN AMAZING OFFER
UP TO 25% Off
On valentine season advertisements*
FROM 10th FEB TO 20th FEB 2023
The Guardian
SUPER BRAND LEADING ENGLISH DAILY
Nipashe
YOUR FAVORITE SWAHILI DAILY
TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON
+255 677 020 701
Email: advertise@guardian.co.tz
Or visit us at Mikocheni light industrial area Opposite ITV / Radio One Dar-es-Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com
*Terms and conditions apply.
Followus: @Theguardiantz



Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Abdulmajid Nsekela (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana kuhusu mkutano maalum ulioandaliwa na tume hiyo kujadili maendeleo ya ushirika na kuweka mkakati wa kuimarisha sekta hiyo. Kushoto ni Makamu Mwenyekiti wa TCDC, Irene Mlola na Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mkurugenzi Mtendaji wa TCDC, Dk. Benson Ndiege. Habari Uk.3. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia acharuka fitina za tenda

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameonya vitendo vya fitina katika zabuni za miradi ya maendeleo, akisema zinarudisha nyuma kasi ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Kutokana na kadhia hiyo, ameziagiza mamlaka za taasisi zinazosimamia utekelezaji wa miradi mahsusi ya umeme kuacha figisu hizo ili utekelezaji wake ufanyike kwa haraka na nchi ipate maendeleo.

Alieleza hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam baada ya kushuhudia hatua ya kwanza ya utiaji saini wa mikataba ya kuimarisha Gridi ya Taifa na kusambaza umeme vijijini ya Sh. trilioni 1.6 itakayoelekezwa kwenye kilimo, viwanda vidogo, vituo vya umeme na vyanzo vya maji.

"Uchaguzi au uteuzi wa makandarasi hawa umefanywa kwa umakini mkubwa sana na ninatambua kuna wenzetu wengi kila mtu alikuwa na mkandarasi wake mkononi, sasa kwa sababu hakufanikiwa kupata tenda fitina ni nyingi, mbio PPRA (Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma), mbio PCCB (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa), kuuzuia ule mradi usifanyike kwa matakwa yake binafsi. Hatutakwenda hivyo.

"Ule muda wa mradi kuchukua mwaka mzima kisa haujapata uamuzi, hapana! Tukiamua fedha ipo, mradi uende ukafanywe, mtu kapata au hakupata, kama hakupata ina maana hakufikia vigezo, kama angefikia vigezo angepata," alionya.

Rais alisema ili miradi hiyo ifanyike na maendeleo yapatikane haraka, kunahitajika uamuzi wa haraka, hivyo kitendo cha watu hao kuzuia kazi za makandarasi walioteuliwa kwa sababu zao binafsi kinarudisha nyuma kasi ya utekelezaji wake.

**VIBALI AJIRA**

Rais Samia aliagiza vibali vya ajira vitolewe haraka kwenye mashirika yanayohitaji kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo kwa kuwa kucheleweshwa kwake kunakwamisha utekelezaji wa haraka.

Mkuu wa Nchi pia aliwaagiza wakuu wa mashirika kutosita kufanya mabadiliko ya kiutendaji pale wanapoona kuna ucheleweshaji wa makusudi wa utekelezaji wa miradi hiyo, ili kuchochea kasi ya utekelezwaji wake.

Vilevile, Rais aliwataka makandarasi walioshinda zabuni katika miradi hiyo, kutokuwa chanzo cha kuikwamisha na kuagiza mamlaka zenye wajibu wa kuwalipa, kufanya hivyo kwa wakati ili utekelezaji wake ufanyike kwa haraka.

"Kama jambo kwenye serikali yetu hatulitaki tuzungumze mpaka tuelewane. Mradi ni wetu, unatekelezwa nchini kwetu, nawe unakuja na masharti yako unayaweka kwenye mradi wetu, hapana!

"Lazima tuzungumze tukubaliane, hakukubaliana, basi wawekezaji wapo wengi," alisisitiza.

Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema serikali imejipanga kuhakikisha kufikia Desemba mwaka huu kila kijiji nchini kiwe kimefikiwa na umeme.

Alisema kuwa hadi kufikia mwaka 2025 ambao ni ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999-2025, Tanzania itakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 5,000 za umeme kulingana na miradi inayotekelezwa.

January alisema kuwa alipoteuliwa mwaka 2021, alikutana na kadhia ya kukatika kwa umeme, hivyo kwa kushirikiana na Shirika la Umeme (TANESCO) walitumia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2019 na kugundua tatizo linasababishwa na uchakavu wa miundombinu na matengenezo hafifu ya mitambo ya umeme na ndicho kinachotekelezwa kwenye miradi hiyo.

Mkurugenzi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Hassan Said alisema serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Ulaya (EU) pamoja na Ufaransa wametenga Sh. bilioni 385 kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa mitatu.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 1,522 mikoa tisa utakaogharimu Sh. bilioni 234.4 na utakaopeleka umeme kwenye migodi na shughuli za kilimo kwenye maeneo 336 ukigharimu Sh. bilioni 115.

Mwingine ni wa kupeleka umeme kwenye vituo vya afya, pampu za maji na mafunzo kwenye maeneo 339 utakaogharimu Sh. bilioni 35.6.

Alisema REA pia itakuwa na miradi mingine mitatu mwaka huu itakayopeleka umeme vijijini, ukijumuisha mitaa 416 iliyoko pembezoni mwa miji katika mikoa minane ukigharimu Sh. bilioni 76.9.

Alitaja mradi wa pili ni wa ujazilizi ambao utapeleka umeme kwenye vitongoji 1,752 ukigharimu Sh. bilioni 293 zitakazotolewa na Benki ya Dunia (WB) na Serikali ya Norway.

Alisema mradi wa tatu utapeleka umeme kwenye mitaa 654 ukigharimu Sh. bilioni 100, fedha za msaada kutoka Shirika la Fedha za Kimataifa (IMF).

Mkurugenzi wa TANESCO, Maharage Chande alisema miradi 26 iliyotiwa saini, itatekelezwa kwa miaka minne, ikiinufaisha mikoa ya Arusha, Manyara, Dodoma, Morogoro, Singida, Tabora, Njombe na Shinyanga.


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM

*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO....30....... OF 20..23......

THE REPUBLIC

VERSUS

OYSTERBAY HOMES LIMITED

To:

Mpina Kaombwe
Oysterbay Homes Limited
Plot No. 1872, Oysterbay Area
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the......02...... day of ......march.......... 20..23.....at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this ...27..... day of ....01.................. 20..23.........

.................................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name.............................................

Signature.........................................

Qualification/Relationship

Date..............................................

217280802

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM

(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO...27...... OF 20...23..

THE REPUBLIC

VERSUS

VICTOR GASPAR

To:

Victor Gaspar
Plot No. 1, Block 6,
Magomeni Mapipa Area
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the.....03... day of ....MARCH.............. 20..23...... at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this ...27...... day of ......JAN................ 20..23......

.................................................
RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name.............................................

Signature.........................................

Qualification/Relationship

Date..............................................

217280802




Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba (kulia), akikabidhi tuzo kwa Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya DCB, Isidori Msaki, kwa kutambua mchango wake binafsi katika kufanikisha maendeleo ya sekta ya fedha nchini, wakati wa sherehe za kumuaga gavana aliyemaliza muda wake, Prof. Florens Luoga (wa pili kushoto) na kumkaribisha gavana mpya, iliyoandaliwa na Umoja wa Mabenki Tanzania (TBA), jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Kushoto ni Mwenyekiti wa TBA, Theobald Sabi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Polisi yanasa watuhumiwa uvamizi wa panya road Bunju

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limewakamata vijana sita wanaodaiwa kujihusisha na vitendo vya kihalifu mitaani, maarufu panya road, kwenye maeneo ya Bunju A na B wiki iliyopita.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye Kituo cha Polisi Mabwepande jana, Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema kukamatwa kwa vijana hao kumetokana na operesheni maalum iliyofanywa na jeshi hilo kwenye maeneo hayo.

Alisema jeshi hilo limefanya kazi ya ziada kuhakikisha wote waliofanya uhalifu, kujeruhi na kuwaibia watu kwenye maeneo hayo wanakamatwa.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha kila kitu kilichoibiwa kinapatikana, huku akisisitiza kuwa kila aliyehusika katika tukio hilo, ataingia katika msukosuko mkubwa wa kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

"Nchi hii inafuata mfumo wa utawala wa sheria na wote waliofanya tukio hilo wataingizwa kwenye hiyo mifumo ili hatua ziweze kuchukuliwa, ukiangalia matukio haya yanafanyika mara nyingi usiku na wanatumia silaha za jadi," alisema.

Kamanda Muliro pia alitoa pole kwa wananchi waliokumbwa na kadhia hiyo, akiwahakikishia jeshi hilo liko imara na kuwahimiza wenyeviti wa serikali za mitaa kuhakikisha kunakuwa na ulinzi shirikishi kwenye mitaa yao.

Alisema wahalifu wanatafuta maeneo yaliyo dhaifu ndiko wanafanya vitendo vya uporaji, kuiba na kujeruhi, akisisitiza wananchi kuachana na fikra kwamba polisi atakwenda kulinda kila nyumba mlangoni.

"Kuna mitazamo ya kusema kwamba hii ni kazi ya askari, kimsingi ni kazi ya polisi lakini kwa kushirikiana na wananchi," alifanua.

HABARI KITAIFA

# TCDC yawaita wadau kuweka mkakati kuimarisha Ushirika

Na Mwandishi Wetu

TUME ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC), wameandaa mkutano maalum wa wadau wa sekta ya ushirika unaotarajiwa kufanyika Februari 27, mwaka huu, kwenye ukumbi wa mikutano wa Makao Makuu ya Benki ya CRDB.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa tume hiyo, Abdulmajid Nsekela katika mkutano na waandishi wa habari uliofanyika Makao Makuu ya Benki ya CRDB jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wa TCDC, TFC pamoja na wadau wengine wa sekta ya ushirika.

Nsekela alisema mkutano huo unalenga kuwaleta pamoja wadau wa sekta ya ushirika ili kujadili maendeleo ya ushirika na kuweka mkakati wa kuimarisha Sekta ya Ushirika nchini.

Alitoa rai kwa wadau wote wa Sekta ya Ushirika kuitikia wito wa kushiriki mkutano huo kwa kuwa mawazo yao ni muhimu katika kuboresha mfumo wa Ushirika.

“TCDC imedhamiria kuboresha mfumo wa ushirika kuwa wa kibiashara na wa kisasa zaidi ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika sekta mbalimbali, na kuongeza mchango wa sekta hii katika kupambana na umaskini pamoja na kukuza uchumi wa nchi,” alibainisha Nsekela.

Aliongezea kuwa kamisheni inaweka nguvu katika uanzishwaji wa mfumo wa kidijitali kuongeza ufanisi kwa vyama vya ushirika, kuimarisha taasisi zinazohusika na usimamizi, kutoa elimu juu ya dhana ya ushirika ili kuongeza ushiriki wa sekta mbalimbali zaidi ya kilimo na kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika.

“Pamoja na hayo katika mkutano huu tutakwenda pia kujadili mifumo ya masoko, usimamizi na matumizi ya mali za vyama, vyama kujiendesha kibiashara, mitaji kwenye vyama vya ushirika, taswira ya Ushirika kwenye jamii. Maazimio yatakayofikiwa kupitia mkutano huo yatapaswa kutekelezwa ipasavyo na kila mdau,” alisisitiza.

Nsekela ambaye alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa TCDC miezi michache iliyopita, pia aliishukuru serikali chini ya Rais Dk. Samia Saluhu Hassan kwa miongozo na jitihada kubwa zinazofanyika kuimarisha Ushirika na kuahidi kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Kilimo katika kufanikisha malengo waliyojiwekea.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mkurugenzi Mtendaji wa TCDC, Dk. Benson Ndiege, alisema katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na uboreshaji mkubwa wa Sekta ya Ushirika, hivyo kupaua wigo wa Ushirika kwenye sekta mbalimbali, kuongezeka kwa mitaji kwenye vyama na kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya serikali hususan katika Sekta ya Kilimo ambapo tozo za mazao 12 zinakusanywa kupitia Ushirika.

Kwa mwaka 2021/22, serikali ilipokea jumla ya Sh. 15,144,077,319.16 zikiwa ni fedha za ushuru unaotokana na zao la korosho uliolipwa na vyama vya TANECU, MAMCU, RUNALI, LINDI MWAMBAO, TAMCU na CORECU.

Vilevile, jumla ya Sh. 1,041,957,051 zimepokewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ushuru kutoka Vyama vya Ushirika vya KDCU na KCU kupitia zao la kahawa.

“Katika kipindi cha mwaka 2015 hadi 2022 tumeshuhudia wanachama wa ushirika wakiongezeka kutoka milioni 2.4 hadi milioni saba, lakini kumekuwa na uwezeshaji mkubwa wa masoko kupitia mfumo wa ushirika, bila kusahau ongezeko la viwanda vya ushirika ambavyo vimekuwa vikisaidia kuongeza thamani kwa upande wa mazao,” alibainisha.

Dk. Ndiege alisema pamoja na mafanikio hayo, kazi kubwa inahitajika kufanyika ili kuufanya Ushirika kuwa na tija zaidi katika maendeleo ya wananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla, hivyo akawataka wadau wote wanaohusika na Sekta ya Ushirika kuhudhuria mkutano huo utakaofanyika Februari 27, mwaka huu.

Baadhi ya wadau wanaotarajiwa kushiriki mkutano huo ni Vyama Vikuu vya Ushirika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU).




Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Abdulmajid Nsekela



## HABARI KITAIFA

# Tani 23 mbegu alizeti zatolewa kwa wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imesambaza tani 23 za alizeti kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Geita na Halmashauri ya Mji wa Geita kwa lengo la kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo na jamii ya wakulima 5,875 wanaozunguka mgodi huo.

Katika msaada huo, Halmashauri ya Wilaya ya Geita imepata tani 13.8 na Halmashauri ya Mji wa Geita imepewa tani 9.1 ikiwa ni mwendelezo wa mpango wa kampuni hiyo tangu mwaka 2015 kuwasaidia wakulima ambao kwa kiasi kikubwa awali walitegemea kutumia mashamba yao kulima zaidi mahindi, mihogo, karanga na malisho ya mifugo.

Mabadiliko katika mazao yanayolimwa yalilazimisha kuwapo programu maalum ya kuwajengea uwezo ikiwa ni sehemu ya mipango ya Mgodi ya Mazingira ya Kijamii na Kiutawala (ESG) kwenye eneo hilo ili kutoa elimu na mbinu bora kwa wakulima wadogo.

Kutokana na mabadiliko hayo, kulianzishwa kwa kilimo cha alizeti kwa msaada wa kitaalamu, ukiihusisha Taasisi ya Kilimo ya Cholima, shirika la utafiti wa kilimo linaloshirikiana na GGML.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhi mbegu hizo za alizeti kwa wakulima wa Kijiji cha Kasota, Halmashauri ya Wilaya ya Geita, Meneja Mwandamizi wa GGML anayeshughulikia uhusiano, Gilbert Mworia, alisema kampuni hiyo imetumia Sh. milioni 108 kununua alizeti ili kuwanufaisha wakulima 5,875 kutoka halmashauri zote za Mji na Wilaya ya Geita.

Alisema msaada huo unatokana na programu maalum ya kuwajengea wakulima uwezo ikiwa ni sehemu ya mipango ya mgodi huo wa Mazingira ya Kijamii na Kiutawala (ESG) ili kutoa elimu na mbinu bora kwa wakulima wadogo.

Alisema kupitia mpango huo, kulianzishwa kilimo cha alizeti kwa msaada wa kitaalamu kutoka Taasisi ya Kilimo ya Cholima.

"GGML inatamani kunufaisha jamii iliyowakaribisha kwa kuanzisha miradi endelevu ambayo itadumu hata baada ya shughuli za uchimbaji madini kuisha.

"Tunayofuraha kusambaza mbegu hizi wakati wa mvua kwa sababu huu ndio wakati mwafaka kwa wakulima kuanza kukuza mbegu zao," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Kanali Boniphace Maghembe, aliipongeza GGML kwa msaada huo na kuwataka wakulima wa Geita kutumia kikamilifu msaada huo katika kipindi hiki cha mvua.

"Wilaya ya Geita ina watu milioni 1.4 na asilimia kubwa ya watu hawa wanategemea kilimo. Tuna jukumu kubwa sana la kuwahimiza wakulima wetu kutumia mbinu za kisasa za kilimo kwa sababu kinaweza kubadilisha uchumi wetu kwa urahisi," alisema.

Mmoja wa wakulima wa alizeti katika Kijiji hicho cha Kasota, Saakumi Makungu ambaye Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha NYABUSAKAMA, alieleza furaha yake kupokea msaada huo na kusema utaboresha mavuno yao kwa kiasi kikubwa.

Akitoa kihistoria fupi ya kilimo kijijini huko, Makungu alisema kuwa alizeti ilianza kuzalishwa Kasota mwaka 2015 ulipoanzishwa mpango wa pamoja wa kujenga uwezo kati ya GGML na Taasisi ya Kilimo ya Cholima.

"Kwa kuwa mahitaji ya mafuta ya kula yanakua kwa kasi, ni dhahiri mustakabali wa wakulima hawa wanaoungwa mkono na GGML ni mzuri sasa," alisema.


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 11 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

CONSTANCE AFUMWISYE MWALUGAJA

To:

Constance Afumisye Mwalugaja
Mbezi Luis Area
Ubungo Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of March 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of 01 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……

Signature……

Qualification/Relationship

Date……

217280802

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 19 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

ROZMIN ROSHANALI MOLEDINA

To:

Rozmin Roshanali Moledina
Plot No. 161, Saza Street,
Chang'ombe Area, Temeke Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of March 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of 01 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……

Signature……

Qualification/Relationship

Date……

217280802

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 22 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

AMIN HABIB PUNJA

To:

Amin Habib Punja
Plot No. 62, Block M, Magomeni Area,
Kinondoni Municipality
**Dar Es Salaam**

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of March 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me:**

Name……

Signature……

Qualification/Relationship

Date……

217280802

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM *(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 10 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

DUNSTAN ROBERT MMINSE ……ACCUSED PERSON

To:
Dunstan Robert Mminse
Madale Mwisho Area,
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on **ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008**

**YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE** name of the **Republic** to appear in this **Court** on the 02 day of MARCH 2023 at **08:00am** Or so soon thereafter as the case can be heard.

**Here in fail not.**

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the **Prosecution**

**Served Upon Me/us:**

Name……

Signature……

Qualification/Relationship
Date……

217280802


## Upelelezi kesi ya Mwakabibi waiva

**Na Grace Gurisha**

UPELELEZI wa kesi ya matumizi mabaya ya madaraka inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Lusibilo Mwakabibi na mwenzake Edward Haule, upo kwenye hatua za mwisho kukamilika.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Wakili wa Serikali, Monica Ndakidemi, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ilipofikia.

Kutokana na taarifa hiyo, kesi hiyo iliahirishwa hadi Machi 15 mwaka huu itakapotajwa tena. Kesi hiyo ya mashtaka mawili ya uhujumu uchumi, ipo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Evodia Kyaruzi wa mahakama hiyo.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa hao walitenda kosa kati ya Machi mwaka 2020 na Machi 2021 ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam.

Katika shtaka la matumizi mabaya ya madaraka, inadaiwa kuwa katika kipindi hicho, Mwakabibi akiwa ameajiriwa kama Mkurugenzi na Mratibu wa mradi wa DMDP, walitekeleza ujenzi wa Kituo cha mabasi cha Buza kwenye kiwanja kilichoko Buza kinachomilikiwa na Kanisa la Anglikana bila ruhusa.

Katika shtaka la matumizi mabaya ya ofisi, inadaiwa washtakiwa hao kwa makusudi walitumia madaraka yao vibaya kwa kwenda kinyume cha Sheria ya Ardhi.

## HABARI KITAIFA

# Watendaji wa kata wanyooshewa kidole



**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amewaonya watendaji wa kata kuacha kuwa miungu watu na kuonea wananchi, akisema wamekuwa wahusika wakuu wa ukiukwaji wa maadili ya kazi zao.

Dk. Mpango (pichani) amesema tuhuma nyingi zinazoendana na uonevu kwa wananchi wahitaji, mamlaka za juu za serikali zimegundua mzizi mkuu uko kwa watendaji hao wanaohusika na wananchi moja kwa moja.

Alitoa kauli hiyo jana jijini hapa wakati wa hafla ya kukabidhi magari kwa Mameneja wa Mikoa na Wilaya wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na pikipiki kwa watendaji wa kata.

Alisema amepata taarifa baadhi ya watendaji hao hawafanyi vikao na wananchi, wajipa hadhi ya miungu watu, hivyo akawaelekeza kubadilika mara moja, wawajibike kwa weledi, uaminifu na kutimiza majukumu yao.

"Simamieni sheria, lakini msionee watu! Sisi huku juu tunaletewa tuhuma nyingi za ukiukwaji wa maadili ya viongozi wa umma ambazo zinafanywa na baadhi yenu maofisa watendaji wa kata," alisema.

Pia aliagiza wakurugenzi wa halmashauri kufuatilia tuhuma hizo na kuchukua hatua stahiki za kisheria na kinidhamu.

Makamu wa Rais aliwataka wakurugenzi hao kugawa pikipiki kwa kuzingatia kata zenye upekee zaidi hasa za pembezoni na zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Ninataka pikipiki hizi tunazogawa leo (jana) zitumike kuwafikia wananchi kwa urahisi, kuwasilikiza kuwahudumia na si kwa manufaa yenu binafsi. Pikipiki zitunzwe vizuri na kufanyiwa matengenezo kwa wakati kwa lengo lililokusudiwa, pikipiki hizi zitakapotumika kwa muda fulani wakopeshwe kwa utaratibu utakaoonekana unafaa," aliagiza.

Pamoja na hayo, alisema serikali haitavumilia viongozi waliokaribu na wananchi, maslahi yao hayapewi kipaumbele na kuwahimiza wakurugenzi wa halmashauri kutenga bajeti za kutosha za kutatua kero zinazowakabili watendaji wa kata kwenye utekelezaji wa majukumu yao.

"Fedha za mafuta na matengenezo zitengwe kila mwezi kwa ajili ya vyombo hivi," aliagiza.

Waziri wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, alisema Rais alikubali pendekezo la kutumika Sh. bilioni 2.9 za mgawo wa kodi ya majengo za kuanzia Julai 2021 hadi Februari 2022 ili kununua vitendea kazi hivyo kwa watendaji wa kata.

"Mgawo huu ni wa kwanza na ni wa miezi saba, tunasubiri hiyo migawo mingine tutafanya makubwa," alisema na kubainisha kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/23, TARURA itanunua magari 47. Kati yake, 26 yatapelekwa Ofisi za Sekretarieti za Mikoa kwa ajili ya usimamizi wa kazi za barabara.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alisema kuwa hadi kufikia Januari 31 mwaka huu, ndani ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, zimetolewa ajira 55,249.

Alisema katika bajeti ya 2022/23, zimetengwa ajira 30,000 na kipaumbele kitakuwa kwenye sekta ya afya msingi, elimu msingi na wahandisi wa TARURA.


CRB CONTRACTORS REGISTRATION BOARD TANZANIA

**A CALL FOR CONTRACTORS ASSISTANCE FUND'S DEFAULTERS TO APPEAR BEFORE THE CONTRACTORS REGISTRATION BOARD**

Contractors mentioned hereunder are instructed to appear at the **Contractors Registration Board's Head Office,** which is located at the **Mkandarasi Place, 1st & 2nd Floor, Plot No. 5, Block A, NCC Link, Dodoma City on Tuesday, the 7th day of March, 2023 at 10:00 am** without fail to discuss issues with regards to defaulting of the Contractors Assistance Fund (CAF):

| | |
|---|---|
| AHMED RAJAB, NINA JIHADHAR KINGO & JOHN MOSSES MBWANA<br>DIRECTORS<br>MAJOR CONSULTANTS LIMITED<br>P.O. BOX 80152<br>**DAR ES SALAAM** | JAMES G. KASOBI & ASHA G. MASAGA<br>DIRECTORS<br>CAPITAL NETWORK LIMITED<br>P.O. BOX 947<br>**TABORA** |
| EDWIN BATEGELEZA & BATEGELEZA E. JEREMIAH<br>DIRECTORS / SHAREHOLDERS<br>BAGENZI ASSOCIATES COMPANY LIMITED<br>P.O. BOX 16095<br>**DAR ES SALAAM** | FRANKLIN PETER LAUWO, AYUB HUBERT BAHATI & PETER ATHANASIO LAUWO<br>DIRECTORS<br>RANKY INFRASTRUCTURE & ENGINEERING LIMITED<br>P.O. BOX 46006<br>**DAR ES SALAAM** |

Failure to appear at the place and on the date herein specified shall amount to blatant breach of lawful instructions, and thus the Board shall proceed to take appropriate Legal and/or Regulatory Action(s) without further recourse.

**ISSUED BY**
**REGISTRAR**

217278502



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUOMBA RIBA KWA UTOAJI WA Ghala/Karakana/Eneo la Kupanga**
**REF ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0022**

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za Awali za ujenzi wa Gati na Kituo cha Upakiaji katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inawaalika wasambazaji waliohitimu kueleza nia yao kwa utoaji wa huduma za:

- **Ghala/Karakana/Eneo la Kukodi**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.
Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**
- Angalau 10000 sqm kipande kimoja cha ardhi kwa ajili ya semina, ghala, yadi ya kufanyia majenzi ya zege.
- Eneo lazima liwe na uzio aidha wa ukuta wa tofali au zege.
- Eneo lazima liwe safi na tambarare
- Eneo lazima liwe na lango pana (zaidi ya mita 8 au geti linaloweza kuongezwa)
- Eneo lazima liwe na huduma ya maji na umeme.
- Lazima kuwe na barabara sahihi ya kufika kwenye eneo, isipungue upana wa mita 8 (ikiwezekana karibu na barabara kuu)
- Dakika 20 (kilomita 10) kutoka bandari ya Tanga

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:
- Huu ni wito kwa kuonyesha maslahi au nia (EOI), umekusudiwa kutoa muongozo kwa watoa huduma kuonyesha uwezo na uzoefu kwa kutoa huduma kupangisha maeneo kwa namna itakayokidhi matarajio ya BBN Limited.
- Wasifu wa kampuni na uthibitisho wa rasilimali za kutosha za kifedha na zenye uwezo kutekeleza kandarasi husika
- Cheti au Hati safi ya mlipa kodi ya kampuni ya mwaka uliopita 2022
- Leseni ya biashara au Uthibitisho kutoka kwa mamlaka husika kuthibitisha uhalali wa kufanya biashara ya kupangisha.
- Wasifu wa shirika unaonyesha wazi miaka ya uzoefu katika biashara ya uwakala wa mali isiyohamishika
- ISO 9001:2015, ISO 14001:2015
- Kuzingatia kanuni za petroli za matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi, unapendekezwa zaidi.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa barua pepe na viambatanishi Size: 20 MBs & Hati zote lazima ziwasilishwe katika lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 28 Februari 2023 , 18:00hrs Saa za Tanzania.**

Kichwa cha barua pepe kinapaswa kuwa: **ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0022 (Nambari ya marejeleo ya EOI iliyotajwa kwenye kichwa)"**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini kabisa yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

2172801102



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE — BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI KWA UTOAJI WA Makontena**
**REF ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0114**

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za awali za ujenzi wa Gati na Kituoa cha Kupakilia katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inawaalika wasambazaji wanaoweza kueleza nia yao kwa ugavi wa:

- **Kontena za Modula, Kontena za Ofisi/Kontena za Vyoo & Mabafu/Kontena za kuhifadia Mafuta & Vilainishi.**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwa Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**
- Kontena mpya au zilizotumika zilizoundwa kwa matumizi ya Ofisi (Flat Pack Office building)
- Kontena za Ofisi (Flat Pack Office)/kontena za vyoo na Bafu/Kontena za kuhifadhi mafuta ft 20 na ft 40.
- Ugavi na kusanikisha makontena tayari kwa matumizi yakiwa na huduma zote ikijumuisha, lakini sio tu, Mitambo, Umeme, mabomba ya maji, vifaa vya matumizi na rangi.
- Makontena kwa ajili ya matumizi ya huduma ya choo na bafu yawe na vitu vyote (mabomba, beseni la kuogea, vyoo n.k)
- Vyombo vinapaswa kuwa tayari kutumika (plug and play).

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:
- Huu ni wito kwa kuonyesha maslahi au nia (EOI), umekusudiwa kutoa muongozo kwa watoa huduma kuonyesha uwezo na uzoefu kufanya ugavi wa makontena kwa namna itakayokidhi matarajio ya BBN Limited.
- Wasifu wa kampuni na uthibitisho wa rasilimali za kutosha za kifedha na zenye uwezo kutekeleza kandarasi husika.
- Cheti au Hati safi ya mlipa kodi ya kampuni ya mwaka uliopita 2022
- Leseni ya biashara au Uthibitisho kutoka kwa mamlaka husika kuthibitisha uhalali wa kufanya biashara husika ya ugavi wa makontena.
- Wasifu wa shirika unaonyesha wazi miaka ya uzoefu katika biashara ya ugavi na utengenezaji wa makontena kwa ajili ya matumizi mbalimbali
- ISO 9001:2015, ISO 14001:2015
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli na matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Wasambazaji na Watoa Huduma wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi, unapendekezwa zaidi.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji na yana uwezo wa kutoa huduma yanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu barua pepe kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi: 20 MBs & Hati zote lazima ziwasilishwe katika lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 28 Februari 2023, 12:00 jioni, Saa za Tanzania.**

Mada ya barua pepe inapaswa kuwa: **ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0114 (Nambari ya kumbukumbu ya EOI iliyotajwa kwenye kichwa)"**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka :** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

2172801102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Angalizo la Rais kwenye zabuni, ujumbe kisheria

**FILIMBI** dhidi ya mapengo kwenye maslahi ya umma imepigwa, huku aliyetoa sauti ya kimamlaka na inayotetema, isiyotaka masihara kwa maslahi ya umma, ni Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa tafsiri yoyote, ni kauli inayomaanisha na kutaka jibu moja tu la mabadiliko kuelekea kwenye kanuni, taratibu, sheria, taaluma na maadili kwa fani yote inayohusu ununuzi, ugavi na utunzaji wa bidhaa, pia huduma mbalimbali.

Rais Samia aliamua kutoa angalizo hilo jana alipokuwa kwenye tukio la kikazi na watendaji wake, kutia saini mikataba ya zabuni za Shirika la Umeme (TANESCO), Dar es Salaam.

Alitumia fursa hiyo kwa kuweka bayana anachokifahamu kinagaubaga kuhusu urasimu na mchezo mchafu, mwenyewe akitumia msamiati 'fitina kwenye zabuni', ikibeba salamu tarehe ya jana iwe mwanzo na mwisho kote kwenye maslahi ya umma, utendaji serikalini ukinyooshewa kidole maalum.

Kwa kurejea agizo hilo, maana yake papo kwa hapo kunahitajika mabadiliko makubwa na ya haraka kutoka kwa watendaji, hasa wa serikalini 'kazi iendelee' kwa wao kubadilika kimaadili na kiuwajibikaji kwa matendo na kitaaluma.

Ambacho amekielekeza kidole Rais Samia, kina mengi na historia ndefu, si kuishia tu kwenye zabuni, bali pia uchafu uko kwenye ununuzi, usalama wa bidhaa zinavyotunzwa ghalani na namna zinavyogawiwa kwa walengwa.

Hata ikirejewa katika taaluma hiyo ya ugavi ambayo sasa imeboreshwa kimataifa kutoka tafsiri ya 'ununuzi na ugavi', sasa imefika kwenye menejimenti ya mnyororo wa ugavi (Supplies Chain Management).

Katika kila alichokisema Rais Samia jana, taaluma hiyo kwenye hatua yake ya kwanza hubeba dokezo linalodumu kila ngazi, wenyewe wanataaluma wanaliita '5R'; ujumbe wa mambo makuu matano yanayotakiwa yasimamiwe kwa usahihi wakati wote.

Hayo ni kwamba ama huduma au bidhaa ipatikane kwa usahihi kwenye viwango vyake, idadi sahihi, kutoka vyanzo vinavyotakiwa, kwa muda na bei sahihi.

Maana yake nini? Rais Samia amewachukulia hatua wahusika kiutawala kwa ngazi ya juu, kimenejimenti na ndani ya ulingo wa taaluma yao.

Ni suala ambalo linatanua tafsiri pana, hata kwa kurejea kanuni ya kiaskari kwamba ombi la mkuu ni agizo linalopaswa kutekelezwa hata kufanya atakayeenda kinyume cha maelekezo ya Rais, anakuwa amekosa kisheri na kimaadili.


Sababu nyingine inayoelekeza uzito mkubwa kwenye agizo hilo la Rais, ni kwamba utoaji zabuni ndiyo njia sahihi kitaifa na kimataifa, kitaaluma na kiutawala kufanikisha huduma na mipango ya utendaji kiserikali na utawala wa umma.

Pia jana, kukashuhudiwa agizo lingine la kitaifa kutoka kwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, ambalo lina unasaba wa moja kwa moja hasa katika lengo lake, pale naye akawanyooshea maofisa watendaji wa kata kwamba hawapo sawasawa katika kuwajibikia umma kwa kujifanya ni miungu watu katika utendaji wao.

Vivyo hivyo, watendaji hao ambao kitaaluma wanazama zaidi katika stadi za rasilimali watu, taaluma yao inawafunga katika kanuni za kuwajibika, pia sheria, sera na kanuni za utumishi wa umma, pasipo kusahau mwongozo mkuu wa kijeshi uliotajwa awali.

Kimsingi, kidole cha Rais Samia kilielekezwa katika mfumo wa kuhudumia umma kwenye mahitaji, kile cha Dk. Mpango akakielekeza kwenye mwenendo wa moja kwa moja wa wahusika wanaouhudumia umma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Vyama vionekane kuanza mikutano

**TANGU** kutenguliwa kwa zuio la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, baadhi ya vyama vimeshazindua rasmi mikutano katika mikoa mbalimbali, huku vingine vikisuasua.

Ambavyo vimeshazindua mikutano hiyo ni CCM, CUF, CHADEMA na ACT-Wazalendo, viongozi wake wameshatengeneza ratiba ambazo zitatumika katika kufanikisha kuwafikia wanachama.

Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 na marekebisho yake ya mwaka 2019, ibara 5.1 (1), inaeleza haki za chama kuwa ni pamoja na kutafuta wanachama na kungwa mkono na wapigakura.

Utenguaji wa zuio hilo, ni fursa kwa vyama vya siasa kujitokeza kwa wingi kufanya mikutano hiyo, ili kutafuta wanachama na kuungwa mkono na wapigakura badala ya kukaa kimya.

Ikumbukwe kuwa hadi sasa kuna vyama vya siasa 19 vyenye usajili wa kudumu, ambavyo vingekuwa vina pilika za mikutano ya hadhara, lakini vingi ni kama havipo kwa kutochangamkia fursa ya kufanya mikutano. Kitendo cha kutofanya mikutano, kinaweza kusababisha vyama hivyo kukosa wanachama, kutokana na ukweli kwamba, mikutano ya hadhara njia mojawapo kuvifanya vijulikane kwa wananchi.

Vilevile, vyama hivyo vina wajibu wa kutoa elimu ya uraia na ya uchaguzi kwa wananchi, lengo likiwa ni kuwajengea uelewa mpana kuhusu masuala ya uchaguzi ili watumie haki yao kuchagua kiongozi wanayemtaka.

**Vilevile, vyama hivyo vina wajibu wa kutoa elimu ya uraia na ya uchaguzi kwa wananchi, lengo likiwa ni kuwajengea uelewa mpana kuhusu masuala ya uchaguzi ili watumie haki yao kuchagua kiongozi wanayemtaka.**

Inawezekana vyama ambavyo havijaanza mikutano vinakabiliwa na ukata, lakini ikumbukwe kuwa vinatakiwa kuwa na vyanzo halali vya mapato, ambavyo yataviwezesha kujiendesha.

Tangu mwanzoni mwa miaka ya 90 wakati mfumo wa vyama vingi uliporejeshwa nchini, ni muda mrefu ambao vyama vingeutumia kujiweka sawa kwa kubuni miradi mbalimbali ya kuvisaidia kujiendesha. Masharti ya upatikanaji wa ruzuku kwa vyama vya siasa, yangekuwa ni chachu ya kuwafanya viongozi wa vyama hivyo, kubuni miradi ikiwamo hata ya kuuza sare za chama, fulana, kofia, kadi na vitu vingine.

Mwisho wa uchaguzi ndio mwanzo wa mwingine, kampeni zisizo rasmi ni jambo la kawaida, hivyo maandalizi, kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2024 na 2025 yanatakiwa kuwa yanaendelea sasa.

Imekuwa ni kawaida kwa baadhi ya vyama kuibuka wakati wa kampeni za uchaguzi bila kuwa na maandalizi yoyote. Ninadhani kampeni za aina hiyo haziwezi kuwashawishi wananchi wakavutika nazo.

Hivyo, njia bora ambayo ingetumiwa na wanasiasa, ni fursa ya kuwapo kwa mikutano ya hadhara ingekuwa ni nafasi nzuri kwa viongozi wa vyama vya siasa kuweka mipango ya kuwawezesha kufanya mikutano hiyo. Msajili hakutaka kutaja majina ya vyama hivyo ambavyo tayari vimeandikiwa barua lakini alitaja makosa kuwa baadhi havina ofisi za kudumu Tanzania Bara na Visiwani au upande mmoja na vingine havina anuani ya posta.

Msajili wa Vyama vya Siasa alishawahi kutaja kasoro za baadhi ya vyama ambazo zinaweza kusababisha vikafutwa kuwa ni pamoja na kukosa viongozi wa kitafa kutoka pande mbili za muungano na pia havina bodi ya wadhamini iliyosajiliwa kwa Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (Rita).

Kasoro nyingine ni kutokuwa na orodha ya wanachama wa chama husika, kwa kuwa ni muhimu kila chama kuwa na orodha ya idadi ya wanachama wake, lakini vingine kutokuwa na ofisi.

Kwa kuwa vyama vilivyoko vya CCM, CUF, CHADEMA, NCCR-Mageuzi, UMD, NLD, UPDP, TLP, NRA, ACT- Wazalendo, CHAUMMA, ADC, TADEA, DP, SAU, AFP, CCK, UPDP na DEMOKRASIA MAKINI, ni imani yetu kuwa vinakidhi vigezo, kwa hiyo vyote vingejitokeza kufanya mikutano.

Zaidi ya miaka mitano, vyama vya upinzani vilikuwa vikilalamika vikitaka kuwapo kwa mikutano ya hadhara, Rais Samia ameruhusu, lakini cha kushangaza ni vichache, ilivyojitokeza kufanya mikutano hiyo.

## Wapata mbinu kuyaboresha maisha bodaboda

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam (CMPD) kimebainisha mkakati wake mpya wa mapinduzi ya kiutendaji unaofahamika kama 'Boda Mpya' unaolenga kuboresha maisha ya wanachama wake katika nyanja mbalimbali, zikiwamo kiuchumi, kitaaluma na kijamii.

Akizungumza kwenye Mkutano wa Kamati Tendaji ya chama hicho uliohusisha viongozi wa wilaya na mkoa jijini juzi, Mwenyekiti wa CMPD, Michael Massawe, alisema kupitia mkakati huo ambao tayari umeanza kutekelezwa, chama kimejipanga kushirikiana na wadau mbalimbali waliobobea katika nyanja za sheria, TEHAMA, bima, habari na mawasiliano pamoja na taasisi za fedha nchini ili kuleta mabadiliko yanayokusudiwa.

"Ili kuhakikisha mabadiliko haya yanafanikiwa, tumeona tuwekeze nguvu zaidi katika kuwajengea uelewa viongozi wetu katika ngazi zote kuhusu mkakati huu kuanzia kwenye vituo, kata, wilaya hadi ngazi ya mkoa na kwa kuanzia tumeanza na hawa wa ngazi ya mkoa na wilaya zote za mkoa wa Dar es Salaam kisha tutashuka chini zaidi katika ngazi za kata na vituo," alisema.

Massawe alitaja mikopo ya pikipiki za miguu mitatu (bajaj) pamoja na pikikipi za kawaida inayotolewa bila dhamana kwa wanachama wa chama hicho kupitia benki kuwa ni moja ya mafanikio makubwa kupitia mkakati huo ambapo hadi kufikia sasa zaidi ya wanachama 700 wameweza kunufaika na aina hiyo ya mikopo inayodhaminiwa na chama hicho.

Massawe alitaja mpango wa huduma ya mikopo ya viwanja na nyumba kwa wanachama wao inayotolewa na benki kwa sasa ni moja ya suluhisho muhimu kupitia mkakati huo unaolenga kuwahakikishia makazi ya uhakika wanachama hao.

"Kwa upande wa mikopo ya viwanja mwanachama analipa kiasi cha Sh. 2,000 tu kwa siku ndani ya miaka mitatu anakuwa amekamilisha deni. Kwa upande wa mkopo wa nyumba yenye thamani ya Sh. milioni 15 na zaidi mwanachama analipa kwa malimbikizo kidogokidogo katika kipindi cha zaidi ya miaka mitano," alibainisha.

Kuhusu mpango wa bima ya afya ambayo ni hitaji la msingi kwa wanachama hao, Massawe alisema kupitia mkakati huo chama hicho kimefanikisha upatikanaji wa bima hiyo kwa wanachama 650 ambao wanalipa malimbikizo ya Sh. 1,000 kwa siku katika kipindi cha miezi mitatu hadi minne.

Wakizungumza kwenye mkutano huo, Mshauri wa Masuala ya Bima wa Chama hicho, John Serengeti pamoja na Mwanasheria wa Chama hicho, Wakili Jema Clemence, walisema wamejipanga kushirikiana na chama hicho kuwasaidia wanachama hususani kwenye maeneo yanayohitaji utaalamu wa huduma za kibima na kisheria.

# Asakwa akituhumiwa kumbaka na kumuua mke wa mwenyekiti

**Na Titus Mwombeki,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linamtafuta Paschal Kagwa (22), mkazi wa Kijiji cha Kishogo wilayani Bukoba Vijijini kwa madai ya kumbaka mke wa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa aitwaye Khadija Ismail (29) na kumuua.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, William Mwampagale, alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alidai kuwa Khadija ambaye ni mke wa Mwenyekiti wa Mtaa wa National Housing, Kata ya Rwamishenye, Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera, alibakwa na baadaye kuuawa kwa kupigwa na kitu butu kichwani.

"Tukio hilo lilitokea Februari 13, mwaka huu, majira ya jioni mama huyo kubakwa na kupigwa na kitu butu kichwani upande wa kushoto na kumsababishia jeraha kubwa lililosababisha kuvuja damu nyingi na kufariki dunia papohapo.

Baada ya tukio hilo, kijana huyo alitokomea kusikojulikana," Kamanda Mwampagale aliwaambia waandishi wa habari.

Alistidia Dominick, wifi wa marehemu aliyekuwa akiishi naye, alidai kuwa ilikuwa majira ya saa mbili na nusu usiku, akiwa nje ya nyumba yao, alimwona Paschal akiwa anatoka ndani amechafuka na akahisi alikuwa katika hali hiyo kutokana na kazi.

"Baadaye niliingia ndani kisha nikasikia watoto wanapiga yowe, nikawauliza 'kwanini mnapiga yowe?' Mtoto wa marehemu akanijibu Paschal amembaka mama, nikasema 'toka huko wewe mtoto mdogo unajua mambo ya kubaka', ndipo nikakimbia kwenda kufungua chumbani nikakuta anagalagala chumbani yuko uchi, nikamfunika na kanga nikampigia mwenyekiti simu na alipofika tukaingia chumbani tukakuta amelala, kumgusa akawa ameshafariki dunia," alisimulia.

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 12 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

ELIAIKA AMBROSE MANYANGA

To:

Eliaika Ambrose Manyanga
Plot No. 150, Block A
Mbweni Area, Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 02 day of MARCH 2023 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me:

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………

217280802

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 20 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

MICHAEL URIO

To:

Michael Urio
Tegeta Area, opposite the Camel Petrol Filling Station
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 02 day of MARCH 2023 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me:

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………

217280802

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 15 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

OMARY MUHINDI MATAKA……………………ACCUSED PERSON

To:
Omary Muhindi Mataka
Plot No. 317, Mikocheni Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 2 day of march 2023 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 27 day of 01 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………

217280802

---

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM (AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 30 OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

OYSTERBAY HOMES LIMITED

To:

Managing Director
Oysterbay Homes Limited
Plot No. 1872, Oysterbay Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM CONTRARY TO SECTION 22 (4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 02 day of march 2023 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 27 day of JAN. 2023

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me:

Name……………………

Signature……………………

Qualification/Relationship

Date……………………

217280802

# Taarifa 'uchafu' dhidi ya wanafunzi zalishtua jukwaa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KASHFA ya ulawiti na matukio mengine ya ukatili wa kingono kudaiwa kuzihusisha baadhi ya shule za Mkoa wa Kilimanjaro, zilimelishtua Jukwaa la Wanawake na Wasichana Wenye Ulemavu mkoani humo.

Kutokana na kuripotiwa kwa taarifa hizo, wameanza kupita kwenye shule jumuishi kuzungumza na wanafunzi wenye ulemavu kuhusu usalama wao na kuwatia moyo kuendelea kutafuta elimu bila kujali vikwazo wanavyoweza kupitia.

Jukwaa hilo lilianza kazi hiyo hivi karibuni baada ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kuunda timu ya kuchunguza madai hayo Januari 17 mwaka huu.

Waziri huyo alitangaza timu hiyo inayoongozwa na Kamishna wa Elimu nchini na inajumuisha Mwanasheria wa wizara hiyo na Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora.

Akizungumza na Nipashe baada ya viongozi wa juu wa jukwaa hilo kutembelea na kupata taarifa za maendeleo ya elimu kwenye Ofisi ya Ofisa Mtendaji Kata ya Njiapanda na Shule ya Msingi Njiapanda Walemavu, Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Linda Macha alisema:

"Tunafanya kazi ya kuhamasisha jamii kupinga ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wasichana wenye ulemavu, ambavyo wanafanyiwa na tunafanya pia uchechemuzi au ushawishi kwa watu wenye ulemavu, kuangalia matatizo ambayo wanafunzi wanafanyiwa na jamii inayowazunguka kama vile ulawiti, ubakaji, ukatili wa kiuchumi, kimwili na kisaikolojia pamoja na kunyimwa haki zao.

"Tumekuja Shule ya Msingi Njiapanda Walemavu, tumebaini matatizo yanayowakabili wakiwa shuleni na pia majumbani. Tunaiomba serikali ifuatilie tatizo la kukosekana walimu wa elimu maalum kwenye shule hii, ambayo ina wanafunzi wenye uziwi. Walimu waliopo ni wa kawaida."

Mratibu wa Elimu Kata ya Njiapanda, Ambasia Macha, alisema kuwa kwenye kata hiyo wana shule inayojumuisha wenye ulemavu pamoja na wanafunzi wa kawaida, lakini shule haina walimu maalum isipokuwa ina walimu wanaofundisha wanafunzi wa kawaida na ndiyo haohao wanaowafundisha wenye ulemavu.

"Wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia, wao wana shule yao ambako wako bweni hivi sasa wavulana kwa wasichana na wana walimu wao maalum ambao wamesomea na wanawafundisha.

"Kwa Kata ya Njipanda, mwaka jana tulifanya utambuzi kwa watoto wenye ulemavu na walibainika watoto wanane, ambao walikuwa bado hawajafikia umri wa kwenda shule. "Lakini pia kuna waliokuwa wamefikisha umri wa kwenda shule, walishindwa kwenda shule kutokana na kukosa kiti mwendo. Kwa mwaka huu, hatujafanya huo ubainishaji wa watoto wenye ulemavu," alisema.

Kwa mujibu wa Mratibu huyo wa Elimu Kata, mpaka sasa wanafunzi 81 waliopangiwa kujiunga na kidato cha kwanza kwenye Shule ya Sekondari Njiapanda, wameshindwa kuripoti shuleni.

"Kwa upande wa darasa la awali kulingana na matokeo, tumefika asilimia 87, lakini kwa darasa la kwanza, tumeshavuka tuko asilimia 167 wakati kwa kidato cha kwanza, sekondari yetu ya Njiapanda, tulipangiwa wanafunzi 299, mpaka jana nioni wameshiripoti wanafunzi 218," alibainisha.

Akijibu hoja zilizowasilishwa kwake na viongozi hao wa jukwaa, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Njipanda, Elisha Mushi, alisema ofisi yake inajiandaa kuanza kamatakamata ya wazazi na walezi walioshindwa kuhakikisha watoto wao waliochaguliwa kwenda shule wanaripoti kabla ya Januari 9 mwaka huu.

"Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Njiapanda ambao tangu kufunguliwa kwa shule Januari 9 hadi kufikia leo (Januari 29) hawajaripoti, tutawakamata wao na wazazi wao.

"Tutapita nyumba kwa nyumba, hata kwa aliyemficha nyumbani mtoto ili asiandikishwe darasa la awali na darasa la kwanza, kwa sababu ana ulemavu wa aina yoyote, hakuna atakayesalimika," alisema Ofisa Mtendaji huyo.




Meneja wa bia ya Pilsner ya kampuni ya Serengeti (SBL), Wankyo Marando (kulia), akiwasiliana kwa njia ya mtandao na washindi wa droo ya kwanza ya promosheni ya bia hiyo ijulikanayo kama Kapu la Wana, jijini Dar es Salaam juzi, ambapo wateja saba wa Pilsner, walijishindia televisheni za kisasa, simu janja na pikipiki moja. Kushoto ni mwakilishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Salim Mgafi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama Kuu yabariki kifungo miaka 30

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Mwanza imebariki mrufani Maonezi Gabriel kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani kwa kosa la kumnajiri mtoto wa miaka 10 baada ya kuona rufani yake haina mashiko.

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya Jaji Mwanabaraka Mnyukwa baada ya kupitia hoja za kupinga adhabu zilizowasilishwa na Gabriel.

Gabriel alikuwa akipinga hatia na adhabu ya kifungo cha miaka 30 aliyopewa na Mahakama ya Wilaya ya Geita.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Mnyukwa alisema baada ya kupitia hoja za pande mbili, haoni sababu ya kuingilia uamuzi uliotolewa na mahakama ya chini kwa kuwa mashtaka dhidi ya mrufani yalithibitika bila kuacha shaka.

"Mahakama baada ya kupitia hoja za pande zote mbili, imeona hoja za mrufani hazina mashiko, rufani inatupiliwa mbali, adhabu ya kifungo cha miaka 30 gerezani iliyotolewa dhidi ya mrufani iendelee," alisema.

Katika kesi hiyo, inadaiwa mrufani alitenda kosa hilo Julai 15, mwaka 2021 eneo la Katoro wilayani Geita.

Upande wa mashtaka uliita mashahidi sita pamoja na vielelezo mbalimbali kuthibitisha kesi hiyo ambapo mwisho wa usikilizwaji, mrufani alitiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo cha miaka 30 gerezani.

Mrufani hakuridhika na uamuzi huo, alikata rufani Mahakama Kuu Mwanza, akiwa na sababu saba ikiwamo ya mahakama ya chini ilikosea kumtia hatiani na kumpa adhabu hiyo bila kuzingatia utetezi wake wa wazi.

Hoja nyingine ni kwamba upande wa mashtaka ulishindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yake bila kuacha shaka.

# Tume ya uchaguzi kugawa kata zenye watu wengi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeishauri Halmashauri ya Manispaa ya Singida kuzigawa Kata ya Mandewa na Misuna zinazoongoza kwa ukumbwa wa eneo na idadi ya watu inayokadiriwa kuwa zaidi ya wakazi 40,000.

Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa Tume hiyo, Leonard Tumua, akizungumza jana na viongozi wa Manispaa ya Singida, alisema Kata ya Mandewa inatakiwa kugawanywa ili kuwe na idadi zaidi ya vituo vya kupigia kura.

Maofisa wa NEC wamefika Manispaa ya Singida kukagua vifaa kwa ajili ya upigaji kura vilivyohifadhiwa kwenye stoo ya halmashauri sambamba na kutembelea Kata za Mandewa na Misuna ambazo zinakadiriwa kuongoza kuwa ukubwa wa eneo na wingi wa wakazi.

"Umbali, ukubwa na wingi wa watu katika Kata ya Mandewa na Misuna kunaashiria ongezeko la vituo vya kupigia kura na uboreshaji wa daftari la mpigakura," alisema.

Tumua alisema upangaji vituo unapaswa kuendana na taarifa za Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ili kuepuka upotoshaji wa takwimu.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Jeshi Lupembe, alisema suala la kugawa kata hizo mbili tayari limeshatua kwa manispaa na taratibu za kuomba kibali kuzigawa unaanzia kwenye kata husika.

Lupembe alisema tayari Halmashauri ya Manispaa imeanza mchakato wa kufuta vijiji, kazi ambayo inaratibiwa na Mwanasheria wa Manispaa, Bahati Kikoti, Manispaa ya Singida ina jumla ya kata 18, vijiji 19, mitaa 53 na vitongoji 83.

Ofisa Uchaguzi wa Manispaa ya Singida, Edson Ndomba, alishauri kuanza kwa mchakato wa kubaini vituo vipya vya kupiga kura mapema sambamba na vituo vya uboreshaji daftari la mpigakura.

Alishauri suala la elimu kwa mpigakura lipewe umuhimu kwa rika zote ili elimu iwafikie walengwa kwa kina, hasa makundi ya vijana kwenye maeneo yote na hasa yale yenye idadi kubwa ya wakazi na pia kwa kuzingatia ukubwa na umbali uliopo.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Yagi Maulid Kiaratu, alishukuru timu hiyo kutoka NEC na kuwataka kubaini vituo vipya kwa wakati sambamba na kutoa elimu kwa wakazi wa manispaa ili wananchi wajitokeze wakati wa kuboresha daftari la mpigakura.

Mstahiki meya alikiri kuwapo kata zenye maeneo makubwa, idadi kubwa ya wakazi na umbali mrefu na kusema ipo haja ya kuygawa maeneo hayo.





## Mwenyekiti CCM awashukia wawekezaji wababaishaji

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Kiria Laizer, amesema hakuna faida yoyote kwa wananchi wa eneo hilo, kuwakumbatia au kuwa na wawekezaji wababaishaji.

Aliyasema hayo jana, wakati wa mkutano wa hadhara na wananchi wa Kidomunge-Naberera, wilayani humo.

Alisema msimamo wa CCM kwa sasa, hawahitaji wawekezaji wahuni katika sekta mbalimbali ikiwamo ya mifugo, kilimo, madini na maeneo mengine, kwa kuwa lengo lao ni kuhakikisha wanashirikiana na wawekezaji waaminifu kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

"Tunawapenda wawekezaji na tunawakaribisha Simanjiro kuja kuwekeza ila tunataka wawe wakweli na tutashirikiana nao, lakini kwa wawekezaji wahuni, waongo na wadanganyifu hatuwataki kabisa," alisema Kiria.

Aidha, alisema kumekuwapo na baadhi ya wawekezaji wachache waliowekeza katika eneo hilo hasa kwenye kilimo ambao wanashirikiana na wenyeviti wasiowaaminifu kufuja ardhi ya wananchi.

"Unakuta kuna mwekezaji amepata ardhi kiasi cha ekari 3,000 akiwa na nyaraka zisizokuwa za halali na wananchi hawana taarifa yoyote zaidi ya Mwenyekiti wa Kijiji na baadhi ya wajumbe. Watu wa aina hiyo hatuwataki kuwaona wala kuwasikia hapa kwetu," alisema.

Diwani wa Ngorika, Albert Msole, alisema baadhi ya wenyeviti wa vijiji wasiokuwa waaminifu na wanaofuja ardhi wameanza kumchukia Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya kutokana na kupiga vita uuzaji wa ardhi kiholela.

Msole alisema: "Mwenyekiti tupo pamoja na wewe kwenye suala hili, endelea kusimamia na kulipinga kwa nguvu zote nasi tutapiga kelele pamoja na wewe kupiga vita uuzaji wa ardhi holela."

# Wafanyabiashara jela miaka 20 kwa kusafirisha dawa kulevya

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAFANYABIASHARA wadogo wawili waliokuwa wamekamatwa na kushtakiwa kwa makosa ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya bangi na mirungi katika Mkoa wa Manyara, wamehukumiwa kwenda jela miaka 20 kila mmoja.

Wafanyabiashara hao walihukumiwa na Mahakama ya Wilaya ya Babati, kutumikia adhabu hiyo ni Swalehe Mohamed (27), mkazi wa Mdori, Wilaya ya Babati na Yahaya Bakari (37), mkazi wa Ngaramtoni, jijini Arusha.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario.

**Mshtakiwa Swalehe, alikutwa na misokoto hiyo Desemba 29 mwaka jana nyumbani kwake Mdori, akiwa amehifadhi chumbani.**

Kabla ya kusoma kwa hukumu hiyo, Hakimu Kimario, alisema mshtakiwa Swalehe Mohamed, ametiwa hatiani, baada ya mahakama hiyo kujiridhisha kwamba, alikuwa mmiliki wa misokoto 125 ya bangi, sawa na gramu 450.

Alisema mshtakiwa Swalehe, alikutwa na misokoto hiyo Desemba 29 mwaka jana nyumbani kwake Mdori, akiwa amehifadhi chumbani.

Kwa mujibu wa hakimu huyo, mshtakiwa alikiuka Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya, Kifungu cha 15A (1) (2) (C) ya Mwaka 2005 iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2019.

Aidha, mshtakiwa mwingine, Yahaya Bakari (37), Mkazi wa Ngaramtoni jijini Arusha, pia ametiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo cha miaka 20 gerezani, baada ya kuthibitika alikuwa akisafirisha mirungi bunda 247, sawa na kilogramu 94.85.

Mshtakiwa wa pili katika kesi hiyo ya usafirishaji wa mirungi, Frank Mushi (45), mkazi wa Sakina jijini Arusha, yeye anaendelea na kesi hiyo baada ya kukana kuhusika kusafirisha dawa hizo.

Hakimu Kimario, wakati anasoma hukumu, alisema washtakiwa hao walikamatwa Februari 2, mwaka huu katika Kijiji cha Bonga, Wilaya ya Babati, wakiwa wanasafirisha mirungi, kwa kutumia gari lenye namba za usajili T.686AHW aina ya Fuso, mali ya Kampuni ya Kisare.



Mkurugenzi mwenza wa Kampuni ya Franone Mining and Gems Ltd inayochimba madini ya Tanzanite katika Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Vitus Ndakize (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu faida ya ukuta unaozunguka migodi ya madini hayo. Wengine ni wafanyakazi wakiandaa kamba za kutumika mgodini. **PICHA: GIFT THADEY**



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro Baraka Kanunga Laizer akizungumza kwenye moja ya kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo. **PICHA: MTANDAO**

## Baraza la Madiwani lawafuta kazi watendaji kisa tuhuma uuzaji ardhi

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

BARAZA la Madiwani Wilaya ya Simanjiro limewatumbua watendaji watatu wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kwa tuhuma za kushiriki uuzaji wa ardhi kiholela.

Uamuzi wa kuwaondoa Simanjiro, watendaji hao akiwamo Mwanasheria wa Halmashauri hiyo pamoja na watumishi wengine watatu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, ulifikiwa juzi na baraza hilo la madiwani.

Akitangaza uamuzi huo, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Jacob Kimeso, alisema baraza hilo limeridhia watumishi hao wanne wahamishwe vituo vya kazi na kuondolewa kwenye nafasi zao.

Aliwataja waliokumbana na adhabu hiyo ni Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Ofisa Ardhi Mteule, Ofisa Ushirika wa Mamlaka hiyo na Mwanasheria wa Halmashauri hiyo.

Diwani wa Orkesumet, Sendeu Laizer, alisema azimio hilo ni uamuzi wa madiwani, kwa kuwa kamati ya fedha ilikubaliana kuhamishwa kwa watumishi hao.

Naye Diwani wa Mirerani, Salome Mnyawi, alisema migogoro ya uuzaji ardhi kiholela, hususani eneo la Shamba la Maro, imesababishwa na watendaji hao.

Alipoulizwa kuhusu uamuzi huo wa madiwani, Ofisa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Evence Mbogo, alisema kwa muda wa utumishi wake katika eneo hilo, ametekeleza majukumu yake ipasavyo, hivyo hana chochote cha kuzungumza juu ya jambo hilo.



# TAKUKURU yawapa elimu kuhusu utoaji huduma

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

WANANCHI mkoani Kagera wameshauriwa kufahamu taratibu za utoaji huduma katika taasisi mbalimbali hususani kwenye mabaraza ya ardhi, mahakamani na hospitali.

Ushauri huo ulitolewa na Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, (TAKUKURU) mkoani Kagera, Ezekia Sinkala, wakati akitoa taarifa ya taasisi hiyo kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka jana.

Alisema ufahamu huo utasaidia kuondokana na dhana kwamba kila ucheleweshaji wa huduma ni kwa sababu ya madai ya rushwa.

**Kwa kipindi cha miezi mitatu ya mwisho ya mwaka jana kulikuwa na malalamiko 90 na kati ya hayo 65 yalihusu rushwa.**

Sinkala alisema kumekuwa na dhana kwamba kila ucheleweshaji wa huduma kutoka kwa watoa huduma inatokana na madai ya rushwa bila kufahamu kuwa zipo sababu zinazofanya mtu asizipate haraka ikiwamo kupata nakala ya hukumu au mwenendo wa kesi.

"Sababu hizo ninaweza kuwa ni upungufu wa makatibu muhtasi katika mahakama na sehemu nyingine za taasisi wanabandika matangazo sehemu mbalimbali ambayo yanaelezea taratibu za utoaji wa huduma husika," alisema Sinkala.

Aidha, alisema kwa kipindi cha miezi mitatu ya mwisho ya mwaka jana kulikuwa na malalamiko 90 na kati ya hayo 65 yalihusu rushwa na hakukuwa na taarifa iliyohamishiwa idara nyingine.

Alisema malalamiko 25 yalihusu rushwa na yalifunguliwa majarada ya uchunguzi na kati ya hayo 11 yamekamilika na hatua mbalimbali zinatarajiwa kuchukuliwa huku 14 bado uchunguzi unaendelea.

Aliongeza kuwa kuna vipaumbele vilivyowekwa na taasisi hiyo kwa kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu ili kuondoa mianya ya rushwa inayotokana migongano ya utendaji.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Vodacom Tanzania Plc, Philip Besiimire (kushoto), akitazama bidhaa kwenye moja ya duka linalotoa huduma za simu, eneo la Buhongwa, jijini Mwanza mwishoni mwa wiki, akiwa katika ziara ya kutembelea watoa huduma za Vodacom. Kulia ni mmiliki wa duka hilo, Robert Ottaru. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake Shinyanga Vijijini walalamika kufanyiwa ukatili

**Na Neema Sawaka,** SHINYANGA

BAADHI ya wanawake katika Kata ya Didia Halmashauri ya Shinyanga Vijijini wamelalamikia kufanyiwa ukatili kwa kupigwa, huku wengine wakizuiwa kujishughulisha na shughuli za kiuchumi ikiwamo kufanya biashara.

Hayo yalibainishwa wakati wa utekelezaji wa mradi wa kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto unaotekelezwa na waandishi wa habari wa Mkoa wa Shinyanga kupitia Mfuko wa Wanawake Tanzania (WFT).

Akizungumzia tatizo hilo mkazi wa Kijiji cha Didia, Ndalo Kulwa, alisema amekuwa akipigwa na mume wake na kuzuiwa kufanya biashara ya mamalishe ambayo ilikuwa ikiwasaidia kujikimu yeye na watoto wake.

Mkazi mwingine, Ester Juma, aliomba asaidiwe kuondokana na tatizo la kupigwa na mume wake na kuzuiwa kutumia simu.

Alisema anapokwenda kutoa taarifa polisi hapati msaada wowote.

"Tunaathirika kisaikolojia na wanaturudisha nyuma kwenye kujikwamua kiuchumi kwa kutuzuia kufanya biashara ili tuendelee kuwa tegemezi," alisema Ester.

Akizungumzia ukatili wanaofanyiwa wanawake katika eneo hilo, Jackson Maganga ambaye ni Mtendaji wa Kata ya Didia alisema wana wakazi 13, 000 na idadi kubwa ni wanawake ambao ni 7,800.

Alisema amekuwa akipokea kesi hizo ambazo zinatokea ngazi za kitongoji na kijiji na anapobaini matatizo hayo huwachukulia hatua ikiwamo kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria.

Hivyo, aliomba mamlaka mbalimbali kuchukua hatua ili kukomesha ukatili dhidi ya wanawake unaofanywa na wenza wao ambao umekuwa kikwazo kwenye shughuli za uzalishaji wa kiuchumi.

# Makandarasi wakumbushwa kuwa makini ujenzi barabara

**Elizabert Selemani,** SENGEREMA

MAKANDARASI wanaojenga barabara katika Halmashauri ya Buchosha wilayani Sengerema mkoani Mwanza wametakiwa kutengeneza mitaro kwa ajili ya kumwaga maji ili kuepusha barabara kuharibika haraka.

Wito huo umetolewa na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Buchosa, Idama, kwenye Baraza la Madiwani wakati akipokea taarifa ya bajeti ya matengenezo ya barabara za Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Alisema makandarasi wamekuwa wakitengeneza barabara, lakini mvua zinaponyesha zinasombwa na maji kwa sababu ya kukosa mitaro mikubwa ya kupitishia maji.

Akitoa taarifa kwa niaba ya Meneja wa TARURA, Kahabi Moses, alisema Halmashauri ya Buchosa inatarajia kutengeneza kilometa 1,001 ambazo wanazihudumia.

Kwa upande wao madiwani waliomba mkandarasi asipewe kazi nyingi kwa kuwa anashindwa kuzimudu kwa ufanisi.

Aidha, waliomba kufunguliwa kwa barabara ambazo bado hazijafikiwa kwa kuwa zinawahudumia wananchi ambao wanaishi kijijini, kwamba wanashindwa kusafirisha mazao yao kiurahisi.

Pia waliiomba serikali kuzihamishia barabara hizo kwa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), ambazo ni kubwa ikiwamo ya Luchili-Katoma hadi Kalebezo ili ziweze kutengenezeka kwa uharaka.

Kaimu Mkurugezi Mtendaji wa Halmashauri ya Buchosa, Alex Mang'ara, alisema ameyapokea mawazo ya madiwani na kuahidi kuyafanyia kazi.

TARURA katika Halmashauri ya Buchosa imetenga Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kutengeneza barabara kwa kiwango cha changarawe na udongo.



**Makandarasi wamekuwa wakitengeneza barabara, lakini mvua zinaponyesha zinasombwa na maji kwa sababu ya kukosa mitaro mikubwa ya kupitishia maji.**

Ndivyo fedha inavyowatupa mbali wanawake kwenye harakati kisiasa

Ukurasa 12



Ukurasa 14



EVARISTE NDAYISHIMIYE NA MZIGO WA DRC

siasa
JUMATANO FEBRUARI 15, 2023
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

## WAKATI CHONGOLO ANAPOWADAI UWAJIBIKAJI ...

# Watumishi wa umma kujali zaidi maslahi binafsi ni tatizo kubwa

**Na Dk. Felician B. Kilahama**

HIVI karibuni Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, anazungumzia viongozi wa chama na serikali kuwajibika ipasavyo, akasisitiza kwamba viongozi legelege, sasa hawana nafasi.

Ni wakati wa mapokezi ya 'Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa' ya CCM jijini Dodoma, anaposikika akiongea baadhi ya masuala muhimu wananchi wanayotaka kwa viongozi, serikali na chama.

Anawakumbusha kila mhusika kujitathmini ipasavyo maana fursa za kuchekeana zinaelekea kuwa finyu.

Katibu Mkuu anasema Watanzania wengi wanahitaji miundombinu bora, barabara safi na zinazopitika mwaka mzima vijijini na mijini, huduma za maji, elimu na afya zikiwa za uhakika na endelevu.

Anachosema ni sahihi lakini afahamu kuwa wanahitaji kupatikane vitendea kazi vya kisasa katika maeneo ya kutoa elimu na kwenye zahanati, vituo vya afya pamoja na hospitali za serikali na za sekta binafsi.

Ni sawa kuwajibika na kuacha ulegelege kadhalika kukumbuka kuwa Watanzania wanaishi katika dunia ya kidijitali, suala la kuwepo na mawasiliano ya uhakika mijini na huko vijijini leo halikwepeki.

Huduma za mawasiliano zinahitajika zaidi sasa lakini kwa kuhakikisha gharama zake zinakuwa nafuu kwa watumiaji, isiwe ni kukomoana au kutaka watumiaji washindwe kuwasiliana kutokana na gharama za mitandao kuwa kubwa.

Uzoefu unaonyesha kuwa wanaomiliki mitandao ya simu hupata faida kubwa kila mwaka pengine mabilioni ya pesa, wakati huohuo, mitandao pia ikitumia gharama kubwa kwa matangazo ya mara kwa mara kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Kadhalika, huweka matangazo sehemu mbalimbali mijini na vijijini ingawa huko siyo kama ilivyo mijini.

Wakati mwingine, magari yenye vipaza sauti hupita mitaa mbalimbali yakitangaza huduma zinazotolewa na mitandao kama kutangaza huduma na bidhaa mpya ili kuvutia wateja.

Haya yote, yanafanyika kwa kumwongezea gharama mtumiaji wa huduma za mawasiliano na teknolojia hata kama vyombo vya habari pamoja na waigizaji watanufaika kutokana na matangazo, lakini ni vyema itambulike kuwa watumiaji wa huduma hizo wanaobeba mzigo wa gharama kubwa.

Wanapohimiza uwajibikaji swali linajitokeza, kulikoni hali ya mawasiliano kuwa 'mwiba' kwa mtumiaji kutokana na gharama za vifurushi vya kuongea au na matumizi ya intaneti kwisha haraka huku malipo yake yakiwa juu au ndiyo mifumo ya kibepari ilivyo? Hilo nalo linatakiwa liboreshwe wananchi wasiendelee kulalamika.

**KILIMO/UFUGAJI**

Pamoja na hayo, huduma za kilimo na ufugaji zinatakiwa ziboreshwe zaidi ikiwamo kuwapo na wataalamu wa kutosheleza na wanaowajibika ipasavyo na kwamba kila jitihada ifanyike wapatiwe vitendea kazi muhimu kwa sekta zote hususan ni za kipaumbele zenye umuhimu wa kipekee kama elimu, afya, maji, kilimo, mifugo, maliasili na utalii na ustawi wa jamii.

Nchi itaendelezwa na Watanzania wenye moyo, wazalendo na wenye uchungu na rasilimali zilizoko. Uwajibikaji usimamie ardhi ili itumiwe kikamilifu kuzalisha mazao kitaalamu na kwa tija.

Vilevile, wafugaji wakisimamiwa na kuongozwa ipasavyo hawatazurura hovyo kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine kwa lengo la kutafuta malisho na maji kwa mifugo.

Uwajibikaji uwamilikishe maeneo ya kufugia mifugo na wawajibike kuyasimamia na kuyatunza ipasavyo pamoja na kuzalisha bidhaa zitokanazo na mifugo kwa weledi bila kuharibu mazingira.



Daniel Chongolo. **PICHA: MAKTABA**

**IWEPO DHAMIRA**

Katibu Mkuu wa CCM Chongolo, anaposema 'Watanzania wanataka barabara zilizoimarika hadi vijijini, wapate huduma za maji, elimu na afya bila kuangaishwa, analomaanisha ni kweli.

Haya yote yanahitaji watumishi waliodhamiria kuwaletea Watanzania maendeleo endelevu. Wanataka miundombinu imara, mawasiliano yawe rahisi na kwa gharama rafiki.

Wakulima wapate pembejeo za kilimo na mifugo kwa wakati tena kwa bei nafuu, lakini wawepo watumishi wa serikali wanaotimiza wajibu wao ipasavyo bila kusukumwa.

Kujitawala ni kufanya kazi kwa bidii na kutimiza wajibu kwa haki na amani, watumishi wa serikali wachukie rushwa na roho za kupenda mlungula na zawadi bali watende haki kwa wakati wote na kuhudumia Watanzania wote kwa wakati bila ubaguzi.

**KATIBA MPYA JE?**

Kuyatimiza haya yote hakuhitaji kuwa na katiba mpya wala demokrasia kama ilivyo katika nchi zenye maendeleo makubwa kiuchumi na kijamii. Ila cha muhimu zaidi ni dhamiri njema kutoka kwa viongozi wafanya maamuzi na watunga sera.

Katiba au demokrasia vinaweza kuwapo lakini bado kukawa ni kizungumkuti. Pamoja na wengine waliotumikia nchi hii naweza kuungana na mimi. Mfano katika utumishi wangu wa miaka 36 kwenye sekta ya umma, sikuwahi kukumbana na katiba au demokrasia.

Shughuli za umma zilifanyika kwa nia njema kufuatana na sheria na kanuni na zilikuwa zinaboreshwa mara kwa mara ili kutenda haki.

Kinachosumbua nyakati hizi ni roho za ubinafsi na kujipenda zaidi kuliko kumpenda jirani kama unavyojipenda. Maslahi binafsi na migongano ya kimaslahi kwa watumishi wa umma ni changamoto kubwa zama hizi.

Iwapo katiba mpya na demokrasia vitasaidia kuondoa roho hizo miongoni mwa watumishi wa umma na wakawajibika ipasavyo bila kujali maslahi binafsi basi taifa likazane hali iwe hivyo. Kinyume cha hapo, itatuchukua muda mrefu sana kuyashuhudia mambo muhimu ambayo Watanzania walio wengi wana kiu ya kuyaona yamefanyika kama Katibu Mkuu wa CCM anavyoainisha.

Kwa muda mrefu watu wanahangaika na maendeleo ya wananchi lakini kwa kusuasua ikiwamo kudhamiria kusikosuasua na kwa nia njema ya kuona Tanzania yenye maendeleo, hakika tutafanikisha.

Kuna uthubutu na imeshaonekana kuwa inawezekana, sasa ni kuongeza kasi katika kuwaletea maendeleo Watanzania wote mijini na hasa vijijini.

Ni muda wa viongozi wa ngazi zote kuwatumikia wananchi kwa uaminifu na weledi, wakitenda haki kwa faida ya wote. Wakiongozwa na kauli mbiu kuwa sasa Tanzania kumekucha taifa linahitaji maendeleo ya kweli na yenye tija kwa wote.

Baada ya 'mzinga' kufunuliwa, nyuki ni wengi kila mahali wanatafuta malighafi ya kutengeneza asali kuanzia chavua na 'mbochi' au nectar, nini kitatokea iwapo 'ukame' utazidi kuongezeka? Naamini hali ya hewa itakuwa nzuri ili vyama vyote vya siasa viweze kutupa karata zao vikiweka bayana hoja zenye manufaa kwa amani na utulivu wa taifa.



Halima Ibrahim, aliyegombea ubunge Jimbo la Malindi Zanzibar kupitia ACT -Wazalendo 2020. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Ndivyo fedha inavyowatupa mbali wanawake kwenye harakati kisiasa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

USHIRIKI wa wanawake katika uongozi ni moja ya njia bora za kujenga demokrasia endelevu, lakini zinahitajika juhudi kuelimisha jamii ili itambue umuhimu wa mwanamke katika uongozi.

Licha ya kwamba bado kuna changamoto ya ukosefu wa fedha na uwepo wa mfumo dume, jamii ikihamasika itabadilika, anasema Halima Ibrahim.

Halima aliyegombea ubunge Jimbo la Malindi Zanzibar, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, akiwakilisha Chama cha ACT-Wazalendo anaeleza.

Anaongeza kuwa bado kuna safari ndefu ya kuwafikisha wanawake kwenye jukwaa la siasa na kuheshimiwa wanapowania uongozi.

Halima hakufanikiwa kupata nafasi hiyo, anasema licha ya kupambana usiku na mchana misukosuko ikiwamo kukosa fedha, kudharauliwa, kukejeliwa na kudhalilishwa ilikuwa vikwazo kwa mwanamke kupata uongozi.

### FEDHA NI LAZIMA

Halima anaiambia Nipashe kuwa, katika harakati za kugombea uongozi fedha inahitajika kwa sababu uchaguzi ni gharama na wanawake walio wengi akiwamo yeye kipato chao ni kidogo.

Anakiri kuwa bado zinahitajika nguvu za ziada ili kuyafikia malengo yaliyopangwa na hilo litawezekana kama wanawake wenyewe wataungana na kuwa na nguvu kiuchumi.

Anasema wanawake wanahitaji fedha kusafiri na kutafuta kuungwa mkono, wanahitaji kuwa na uwezo wa kuitisha mikutano ya hadhara, kukutana na wajumbe, kuzunguka majimboni na mambo mengi yanayohitaji fedha.

Halima anaona kuwa fedha nyingi zinahitajika kufanya kampeni na pengine hata milioni 10 ili kufanikisha juhudi hizo za kisiasa na kwamba bila kuwa na uchumi imara na fedha mfukoni ni kazi ngumu kwa wanawake kupata uongozi wa kisiasa majimboni.

"Japo mtaji wetu ni idadi ya wapiga kura ambao wengi ni wanawake, lazima tuungane bila ya kujali itikadi za kisiasa anaposimama mwanamama tumuunge mkono na tumchague,"anasema Halima.

Aidha, anasema dhana potofu kuhusu harakati za kumkomboa mwanamke, pia zinachangia kurudisha nyuma malengo ya milennia na siasa za Zanzibar zinachangamoto katika harakati za uongozi kutokana na mitazamo hasi ya dini kwa baadhi ya jamii ambayo asilimia 90 haiwaamini kinamama.

### WALEMAVU TAABANI

Jamila Borafia, anayeishi na ulemavu, haoni, licha ya hali hiyo, aligombea uwakilishi jimbo la Mwanakwerekwe mwaka 2020 kupitia CCM.

Anasema: "Wanawake wenye ulemavu, wanakabiliwa na changamoto nyingi zaidi ikilinganishwa na wanawake wasio na ulemavu katika kugombea nafasi za uongozi."

"Mwanamke mwenye ulemavu akigombea utasikia 'huyu naye anataka uongozi jamani? Atatuongoza nini, ataongozaje wakati haoni? Tuna changamoto nyingi zaidi," anasema Jamila.

Hakufanikiwa kupata nafasi hiyo anasema, lakini anasisitiza kuwa ushiriki wa wanawake wenye ulemavu ni mdogo mno na kukosa uwakilishi wao majimboni.

Anakumbusha kuwa licha ya kipato duni walichonacho wanawake wenye ulemavu, lakini miundombinu sio rafiki katika kugombea nafasi za uongozi majimboni na kwingineko.

Anaeleza kuwa fedha ni muhimu kwa wenye mahitaji maalumu kama yeye kwa sababu watahitaji usafiri muda wote, wasaidizi, huduma nyingine mahususi tofauti na wagombea wengine wenye viungo timamu.

"Jumuiya ya wenye ulemavu kwa kiasi kikubwa imetengwa na maisha ya kijamii na hatuna uwakilishi. Hata kama upo ni mdogo katika mabunge na vyama vya siasa na hivyo kupunguza uwezo wa kushiriki moja kwa moja katika maamuzi yanayoathiri maisha yao."

Jamila anaamini kuwa uwepo wa wanawake wenye ulemavu kwenye siasa ni muhimu ili kukuza haki na ustawi wao katika nyanja zote za jamii ikiwa ni pamoja na maisha ya ndani ya jamii na ya kisiasa.

### WANAHITAJI UTHUBUTU

Jamila na Halima wanaamini kuwa kujengewa uthubutu ni muhimu, wakisema mafunzo waliyopatiwa na Chama cha Wanahabari Wanawake-TAMWA Zanzibar, kabla ya mwaka 2020 yamemsaidia kuwajengea uwezo na uthubutu.

"Mafunzo yale yamenijengea uthubutu mkubwa na kujiamini maana awali sikuwa naweza kusimama mbele ya kundi la watu kuzungumza na kutetea hoja," anasema Halima.

Anaongeza kuwa mafunzo hayo pia yamemwezesha kukishawishi chama chake na kufanikiwa kupita katika mchakato wa kura za maoni za kugombea ubunge jimboni.

Anaongeza"Tanzania ili uwe mgombea ni lazima utoke katika chama cha siasa na hakuna mgombea binafsi hivyo lazima wanawake washiriki. Tuonekane tokea katika ngazi za chini ndani ya chama."

Anasema yupo katika harakati za siasa tangu mwaka 1993 na hakupata kugombea nafasi ya ubunge jimboni hadi 2020 alipojitosa katika jimbo la Malindi.

Hata hivyo, anasema licha ya kukosa nafasi hiyo lakini bado hajakata tamaa na kwa sasa anajiandaa kwa uchaguzi wa mwaka 2025 akigombea tena nafasi hiyo.

Dk. Mzuri Issa Mkurugenzi wa TAMWA Zanzibar, anasema Tanzania imeridhia mikataba na matamko mengi ya kimataifa yanayosisitiza usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wanawake hususan ushiriki wao katika ngazi zote za maamuzi kimataifa, kikanda na hata sera na miongozo ya kitaifa.

Anatoa mfano Azimio na Mpango Kazi wa Beijing, mkataba wa kimataifa wa kutokomeza aina zote za ukandamizaji na dhuluma dhidi ya wanawake, mkataba wa Usawa wa Jinsia wa SADC, pamoja na ule wa Maputo, ambayo inalazimisha kujali usawa wa kijinsia.

Aidha anasema TAMWA na wanaharakati wengine, wanapambana kutengeneza mikakati itakayowasaidia wanawake kutambua nafasi na uwezo wao kwenye jamii, ikiwamo harakati za kisiasa.

Anasema wanaendelea kutoa elimu kwa njia mbalimbali katika kuhakikisha wanawake wanatambua uwezo wao, fursa na namna wanavyoweza kubadili sura ya mfumo kandamizi.

"Tunawashirikisha wanawake kwenye mikoa yote kuona kuwa wanaweza na wanafaa kuwa viongozi. Tunachofanya ni kuwafundisha ujasiri wa kuthubutu lakini bila ya kuwasahau wanaume na viongozi wa dini," anasema Dk. Mzuri.

Aidha, Dk. Mzuri, anasema ni wakati wa wanawake kupambana na mila na desturi zilizopitwa na wakati na kuhimiza kuwapo kwa usawa wa kijinsia kwa uwiano wa 50 kwa 50.

# Darasa la UVCCM kwa vijana laagiza kuacha siasa za porojo



Mjumbe wa Baraza Kuu la UVCCM Taifa, Ramadhan Matola, alipotoa darasa kwa vijana wilayani Ruangwa. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

MJUMBE wa Baraza Kuu la Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Taifa, Ramadhan Matola, anasema wakati huu si wa kuendelea na siasa za porojo, bali vijana wa umoja huo wajikite, katika hoja zitakazoiwezesha CCM kuendelea kubaki madarakani.

Anaeleza nia ya chama kuendelea kung'atuka wakati wa kuhitimisha ziara yake mjini Ruangwa mkoani Lindi, ambako alikwenda kushiriki katika maadhimisho ya miaka 46 ya kuzaliwa kwa CCM zilizofanyika kimkoa wilayani Ruangwa, anapotoa darasa hilo.

Aidha, mjumbe huyo anawataka vijana kuendelea kuishi misingi ya chama hicho ikiwamo kujenga umoja, kupiga vita rushwa na kuulinda Muungano Tanganyika na Zanzibar ambao umezaa Tanzania.

"Huu si wakati wa porojo tena, hivyo ninawaomba vijana tuachane nazo badala yake tufanye siasa za kujenga hoja, ambazo zitasaidia kuifanya CCM iendelee kushika dola na kuisimamia serikali," anasema Matola.

Anasema serikali ya CCM imetekeleza miradi mingi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, reli ya kisasa, kujenga miundombinu ya madaraja na barabara za lami zinazounganisha mikoa yote na hata baadhi ya wilaya.

"Kwa ujumla kuna miradi mingi ya maendeleo, ni vyema vijana tuiseme, ili wananchi waijue, kwani kuna wenzetu wanaojifanya hawaoni, wanaweza kuja na hoja za kudai kuwa serikali ya CCM haijafanya kitu," anasema.

Mjumbe huyo anasema UVCCM wakijenga hoja kwa kusema mazuri yote yaliyofanywa na serikali, itakuwa ni fursa kwa wananchi kuendelea kukiamini chama chetu.

"Ikumbukwe kuwa Rais Samia ameruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, hivyo UVCCM tunatakiwa kusimama imara na kujipanga kujibu hoja badala ya siasa za porojo majukwaani," anasema.

Matola anashauri kuwa yapo mengi yaliyofanywa na yanaendelea kufanyika na kwamba wananchi hawawezi kufahamu bila vijana hao kuwaambia na kuwataka wawe mabalozi wa kusemea mazuri hayo kupitia majukwaa ya mikutano ya hadhara.

Mjumbe huyo anasema UVCCM wakijenga hoja kwa kusema mazuri yote yaliyofanywa na serikali ya CCM, itakuwa ni fursa kwa wananchi kuyajua na kuwafanya waendelee kuiamini na kuipa kura za kishindo iendelee kubaki madarakani.



Vijana wa UVCCM wakifuatilia hotuba ya mjumbe huyo.

Pamoja na hayo Matola anawataka UVCCM kuwa walinzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa kwa kutoa taarifa kwa vyombo vya dola wanapoona inahujumiwa.

"Lakini vijana wa Lindi hatuna budi kumshukuru Rais Samia kwa kuendelea kutuamini, kwa kutupa nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chama na serikalini, hivyo ni muhimu tulinde imani hiyo," anasema.

Kaimu Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Lindi, Pius Pukapuka, anaahidi kwamba vijana wa mkoa huo watafanya siasa za hoja na kuipigania CCM bila kuchoka, ili iendelee kuwa madarakani.

Mwenyekiti wa kundi la vijana wa hamasa Wilaya ya Ruangwa, Halima Legeja, anaishukuru Kamati ya Utekelezaji ya CCM Mkoa wa Lindi kwa kuifanya Ruangwa kuwa mwenyeji wa maadhimisho kimkoa.

Wakati mjumbe huyo anatoa wito wa kujenga hoja badala ya porojo, tayari Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia alishatoa maelekezo kwa wanachama kujiandaa kukosolewa na vyama vya upinzani katika mikutano ya hadhara.

Hapa ni baada ya kuruhusu mikutano hiyo ambayo anawataka wana CCM kujibu hoja badala ya 'kupayuka' majukwaani, huku akisisitiza kuwa chama hicho kimekuja na mwelekeo wa maridhiano.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo wa CCM, maridhiano hayo yanakwenda sambamba na ustahimilivu, mabadiliko na kujenga upya nchi, na kwamba kazi hiyo inatakiwa kufanyika hata kwenye chama.

"Naomba sana, tunapokosolewa tuangalie, yale ya kweli tuyachukue tuyafanyie kazi, yawe makosa yameondoka. Yale ambayo si ya kweli, twendeni tukajibu kwa hoja, lakini kubwa ni ustahimilivu," Rais Samia anakaririwa na vyombo vya habari akisema.

Mwenyekiti anakumbusha kuwa vijana wa CCM wasipokuwa wastahimilivu, watapandishwa kwenye jukwaa kujibu hoja na kushindwa na kubaki kupayuka, ambapo anawataka wajipange.

Anasema hayo katika kilele cha matembezi ya vijana kuadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyoandaliwa na UVCCM huko Unguja, akiwa mgeni rasmi na kuongeza kuwa CCM imejipanga lakini baadhi ya vyama havijipangi, ingawa vinaweza kuja na hoja za kukosoa.

"Twendeni tukafanye mabadiliko ndani ya chama, pia kwenye jumuiya zetu. Yale tuliyoyazoea, ugomvi kati yetu uachwe. Tunakwenda kwenye mapambano ya kisiasa, tunakwenda kutetea nafasi yetu ndani ya nchi hii, tunakwenda kuonyesha kwamba sisi ni chama kiongozi," anasema.

Mwenyekiti huyo anakumbusha kuwa mwaka 2024 kuna uchaguzi wa serikali za mitaa, ambao ni muhimu kwa chama chake, huku akionya kuwa wakienda wamegawanyika, hawatafanya vizuri, hivyo anawataka wawe wamoja.

"Zama za ugomvi, kupigana na kutukanana katika siasa, ziishe, twendeni na hoja za maana, hoja za kujenga. Tuvumiliane tulete maendeleo ya kweli na yenye tija ili tujenge Tanzania mpya yenye maendeleo endelevu," anasema.

EVARISTE NDAYISHIMIYE NA MZIGO WA DRC

# Aanza kuisambaratisha M23, wakuu majeshi EAC wataka kikosi kila nchi

## •Wawapa waasi onyo la mwisho siku 30 waondoke

**Na Mwandishi Wetu**



Kikosi cha askari 750 kutoka Sudan Kusini kikijiandaa kwenda DRC kujiunga na majeshi ya kikanda kuwakabili M23: **PICHA: VOA**

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) Rais wa Burundi Evariste Ndayishimiye, anaanza mwezi Februari kwa kukutanisha wakuu wa nchi wanachama wa jumuiya hiyo kutatua changamoto ya waasi wa M23.

Ni Februari 3, 2023, anapotoa wito wa kuitisha Mkutano wa Kilele wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kumaliza viporo au mambo yanayosuasua ndani ya EAC.

Wakuu wanakutana kuanzia Februari 4, 2023 kujadili jinsi ya kutekeleza juhudi zao (viongozi wa Afrika Mashariki) walizokubaliana nchini Kenya Juni mwaka jana.

Marais kwa kauli moja wanaahidi kupeleka kikosi cha usalama cha kanda kitakachoongozwa na Kenya ili kukomesha mzozo wa mashariki mwa DRC.

Mwenyekiti Ndayishimiye, anafuatilia utekelezaji wa makubaliano hayo baada ya nchi takribani zote kuonyesha nia ya kukubaliana na wito wa kuunda jeshi la kikanda la EAC ambalo litakuwa mashariki mwa DRC.

Viongozi wa EAC waliokutana Kenya jijini Nairobi, wanaahidi kujitolea kuchangia kupatikana amani na maridhiano katika majimbo ya Kivu Kaskazini, Kivu Kusini na Ituri. Rais wa Burundi na mwenyekiti wa sasa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, anaongoza 'Regional Oversight Mechanism' (ROM) au Ujumbe wa Kikanda wa Uangalizi unaoungwa mkono na Umoja wa Afrika pamoja na Umoja wa Mataifa, ukifanyakazi Ukanda wa Maziwa Makuu, ukikusudiwa kufanikisha kukomesha ghasia mashariki mwa DR Congo.

### HATUA ZAANZA

Baada ya Mkutano wa Wakuu wa EAC huko Bujumbura, Wakuu wa Majeshi ya Ulinzi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wameagiza kutumwa mara moja kwa wanajeshi kutoka mataifa wanachama ambao bado hawajajiunga na jeshi la kikanda la kuimarisha amani huko Goma, mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Wakuu hao wa majeshi wanaokutana jijini Nairobi wiki iliyopita sanjari na Sekretarieti ya EAC walifuata maagizo ya wakuu wa nchi yaliyotolewa hivi karibuni baada ya mkutano wa kilele wa Bujumbura wa kuwa na vikosi vyake DRC, kwa kuzingatia muda uliokubaliwa na wakuu wa usalama.

Aidha, wakuu wa majeshi hao wanakubaliana kupeleka wanajeshi katika maeneo yaliyopangwa kwa ajili ya waasi hao kuondoka karibuni na kuweka ulinzi wa raia sehemu zilizoachwa na M23.

Mwenyekiti Wakuu wa Majeshi wa EAC na Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Burundi, Jenerali Prime Niyogambo, anasema kwa pamoja wanaonyesha matumaini kwamba mashauriano hayo yatachangia katika kuleta amani na utulivu wa kudumu mashariki mwa DRC.

"Nina matumaini kuwa kufika kwa kikosi kilichosalia cha Kanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EACRF) kuharakisha vikosi vya kanda kutekeleza majukumu yake," mwenyekiti huyo anasema.

Vikosi vya majeshi ya kikanda vilitumwa kulinda amani lakini bado havijaanza mapambano dhidi makundi ya waasi yenye silaha kwa vile viongozi wa EAC wanapendelea mazungumzo na diplomasia zaidi, wakiamini mapigano kivita ni njia ya mwisho.

Hadi sasa, mrundikano wa mashinikizo dhidi ya M23 na mienendo ya kukosekana usalama iliyosababisha kuuawa kwa askari wa kulinda amani wa Umoja wa Mataifa raia wa Afrika Kusini katika shambulio la helikopta hivi karibuni kunaweza kusababisha mikakati katika mbinu ya kumaliza mzozo eneo hilo.

Baadhi ya mataifa ya EAC yaliyoahidi kupeleka vikosi DRC ni Sudan Kusini inayotuma wanajeshi 750 kujiunga na Kikosi cha Afrika Mashariki.

Wanajeshi hao pamoja na vikosi vya Kenya, Burundi na Uganda, katika kukamilisha juhudi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kukabiliana na ghasia katika eneo hilo na kuleta utulivu nchini.

### ONYO LA MWISHO

Katika hatua nyingine wakuu wa majeshi wa EAC wametoa siku 30 kuanzia Februari 28 hadi Machi 30 kwa waasi wa M23 kujiondoa katika maeneo wanayoyadhibiti, vinginevyo watatoa melekezo mengine.

Agizo hilo linatolewa hivi karibuni wakati walipokutana jijini Nairobi nchini Kenya, ili kutathmini hali ya usalama mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo ikiwa ni hatua za utekelezaji wa agizo la wakuu wa nchi wanachama.

Katika taarifa ya pamoja ya wakuu hao wa majesshi, wanawataka waasi wa M23 kuanza kuondoka katika maeneo ya Kibumba, Rumagambo, Karengo, Kirolirwe na Kitchaga kuanzai Februari 28 hadi Machi 10 mwaka huu.

Aidha, waasi wa M23 wanaokalia maeneo ya Kishishe, Bambo, Kazaroho, Tongo na Mabenga, wamepewa kati ya Machi 13 hadi 20 mwaka huu kuondoka, huku awamu ya mwisho ikipangwa kwa waasi hao kujiondoa, Rutshuru, Kiwanja na Bunagana kati ya Machi 23 hadi 30.

Hata hivyo, kutokana na hali ya usalama kuendelea kuwa mbaya nchini DRC, wakuu hao wa majeshi wamezitaka nchi za ukanda ambazo hazijatuma vikosi vyake Mashariki mwa DRC kufanya hivyo mara moja, huku ikiamuliwa kuwa wanajeshi wa Burundi, watapiga kambi ya Sake, Kirolirwe na Kitchanga.

Vile vile inaeleza kuwa wanajeshi wa Kenya watapelekwa Kibumba, Rumangabo, Tongo, Bwiza na Kishishe, huku wakisaidiwa na wale wa Sudan Kusini huko Rumangabo.

Pia inabainishwa kuwa Jeshi la Uganda yatakuwa Bunagana, Kiwanja, Rutshuru na Mabenga.

Mbali na suala la M23, mkutano huo umetaka kikosi hicho cha jumuiya, kati ya mwishoni na mwezi Machi na Aprili kuanza kukusanya taarifa kuhusu kundi la FDLR na kuyasaka makundi mengine ya waasi kama ADF, RED Tabara, FNL na NAS.

***RFI, VOA, REUTERS***



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Rais Evariste Ndaishimiye wa Burundi.

# Ukosefu elimu ya fedha sababu wananchi kujikwamua kiuchumi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, amesema ukosefu wa elimu ya fedha na biashara kwa Watanzania ni moja kati ya vikwazo vinavyosababisha wananchi kushindwa kujikwamua kichumi.

Amesema katika kipindi cha mwaka jana mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi nchini imetoa mikopo kwa Watanzania milioni 9.8 ambapo wanawake ni asilimia 53, na Sh. trilioni 5.6 zimetumika.

Alibainisha hayo jana jijini hapo, alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za baraza hilo kwa waandishi wa habari.

Alisema ukosefu wa elimu ya fedha na biashara umekuwa kikwazo kikubwa kwa wananchi kushindwa kufikia malengo yao ya kujikwamua kiuchumi.

"Elimu ya fedha na biashara bado ni kikwazo kikubwa kwa wananchi wetu kushindwa kujikwamua kiuchumi wengi wanakopa fedha lakini namna ya kuzitumia hawajui na kujikuta wakiingia katika mzigo wa madeni yasiyokuwa na tija kwao," alisema.

Alisema wanawake wengi wamekuwa wakikopa fedha katika taasisi za kifedha ambazo zimekuwa zikichangia kwa kiasi kikubwa kuwafilisi.

Alisema kutokana na hali hiyo baraza hilo limeshazungumza na Wizara ya Fedha na Mipango kuona namna ambavyo inaweza kuanzisha mitaala ya elimu ya fedha kwa wanafunzi kuanzia shule za msingi ili kuwajengea elimu ya nidhamu ya fedha.

"Watanzania kama tunataka kufanikiwa ni lazima kuwa na elimu ya fedha siyo lazima iwe ya mkopo bali hata fedha yako ya mshahara lazima uwe na nidhamu nayo, na ujijengee tabia ya kuweka akiba mikopo siyo kitu kizuri sana kama hujajipanga nini unataka kufanya,"alisema.

Kadhalika, alisema kama Watanzania watakuwa na tabia ya kujiwekea akiba, wanaweza kuanzisha biashara zao hata bila kutegemea mikopo kutoka katika taasisi za kifedha kwa kuanza na kile kidogo walichojiwekea.

Hivyo aliwataka wananchi kujenga tabia ya kuwa na bima za aina mbalimbali zitakazowasaidia kulinda mali ambazo wamezitafuta kwa muda mrefu.

**Ukosefu wa elimu ya fedha na biashara umekuwa kikwazo kikubwa kwa wananchi kushindwa kufikia malengo yao ya kujikwamua kiuchumi.**

# Hospitali ya Rufani Dodoma yapokea msaada vifaa tiba

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

HOSPITALI ya Rufani ya Dodoma imepata msaada wa vifaa tiba vya mifupa vyenye thamani ya Sh. milioni 400 kutoka Marekani.

Msaada huo ni baada ya hospitali hiyo kufanya vizuri kwenye matibabu ya magonjwa ya mifupa duniani.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Dodoma, Dk. Ernest Ibenzi, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya taasisi hiyo.

Dk. Ibenzi alisema hospitali hiyo ilifanikiwa kupata zawadi ya vifaa hivyo kutokana na kufanya vizuri kwenye utoaji wa huduma ya matibabu ya mifupa kwa mwaka 2021.

Alitaja malengo yao ni kuendelea kutoa huduma hiyo kwa hali ya juu pamoja na magonjwa mengine ili kuokoa maisha ya wagonjwa wanaofika kupata huduma kwao.

**Vifaa hivyo vilishafika hapa nchini na wamekabidhiwa, wanategemea kuanza kuzitumia kwenye hospitali zingine.**

Alisema vifaa hivyo vilishafika hapa nchini na wamekabidhiwa, wanategemea kuanza kuzitumia kwenye hospitali zingine.

Dk. Ibenzi alisema hospitali hiyo imeanza kuzigawa vifaa hivyo kwa Hospitali ya Mount Meru ya mkoani Arusha na Hospitali ya Mkoa wa Morogoro pamoja na hospitali zingine hapa nchini ili kuwasogezea wananchi huduma hiyo huko walipo.

Kadhalika alisema hospitali hiyo ilifanya vizuri kwa mwaka jana na kushika nafasi ya pili nyuma ya hospitali moja ya nchini Cambodia.

Alisema kutokana na uongozi wa serikali hospitali hiyo imefanikiwa kuwa na mtambo wa kuzalisha hewa ya oksijeni ndani ya eneo hilo.

Aliongeza kuwa vitanda 267 vya hospitalini hapo vimeunganishwa na hewa hiyo na kusaidia wagonjwa kupungua kwenye chumba cha wagonjwa mahututi (ICU)

Pia alisema hospitali hiyo ina matibabu ya kibingwa 14 na kuna madaktari bingwa 23 wa magonjwa mbalimbali.

Dk. Ibenzi alisema katika kutoa huduma kwa wagonjwa ikitokea mgonjwa amekosa huduma kwenye duka la dawa ndani ya hospitali hiyo wao wanawajibika kwenda kuitafuta nje ili kumpunguzia usumbufu mgonjwa.

Altaja mafanikio mengine ni kuwa serikali imewapatia vifaa vya vipimo vya mionzi (X Ray) kutoka mashine moja ya kizamani hadi kufikia tatu za kisasa za kidigitali ambazo zinamwesha mgonjwa kupata majibu muda huo.

Alisema mafanikio mengine kwa sasa wana mashine za utra sound saba pamoja na mashine za CT scan tatu.



Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu mafanikio ya baraza hilo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# NCC kukamilisha mwongozo gharama za ujenzi wa barabara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA mwaka wa fedha 2022/2023 Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), limepanga kukamilisha mwongozo wa gharama za ujenzi wa barabara nchini kwa kuandaa gharama za msingi za mkandarasi katika kutekeleza kazi mbalimbali kila mkoa nchini.

Mtendaji wa Baraza hilo, Dk. Matiko Mturi, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya baraza hilo kwa waandishi wa habari.

Alisema jukumu lingine katika mwaka huo wa fedha ni kuandaa mapendekezo ya kuboresha sheria na miongozo inayosimamia ujenzi wa majengo nchini.

Aidha, alisema jukumu jingine ni kusimamia utatuzi wa migogoro inayotokea katika miradi ya ujenzi, kutoa ushauri wa kiufundi kwa wadau mbalimbali wa sekta ya ujenzi.

Kadhalika alisema katika kipindi cha Julai mwaka jana hadi Januari mwaka huu Baraza la Taifa la Ujenzi limefanikiwa kuandaa rasimu ya mapendekezo ya gharama za msingi za ujenzi wa barabara kwa kila mkoa.

Vilevile alisema katika kipindi hicho NCC, imeratibu na kukamilisha matayarisho ya awali ya kuandaa miongozo ya ujenzi wa majengo nchini.

Alisema NCC, imeandaa mafunzo ya kusimamia mikataba ya ujenzi na utatuzi wa migogoro katika miradi ya ujenzi kwa wadau 155 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.



# Mkoa wa Mbeya wapokea mtambo wa kuchoronga visima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WIZARA ya Maji, imeikabidhi Serikali ya Mkoa wa Mbeya seti ya mtambo wa kuchorongea visima wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 900 kwa ajili ya kupunguza tatizo la uhaba wa maji hasa maeneo ya vijijini.

Mtambo huo ulikabidhiwa jana kwa Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera na Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ikiwa ni siku chache tangu serikali ilipoahidi kupeleka mtambo huo.

Mahundi alisema mtambo huo ni miongoni mwa mitambo 25 iliyonunuliwa na serikali kwa ajili ya kuisambaza kwenye mikoa yote nchini na kwamba fedha zilizotumika kununua mitambo hiyo ni zile za mapambano dhidi ya Uviko-19.

Alisema mtambo huo utatumika kuchoronga visima kwenye vijiji vyote vya Mkoa wa Mbeya ambavyo vina tatizo la uhaba wa maji ili kutimiza lengo la serikali la kumtua mwanamke ndoo ya maji kichwani kwa kuhakikisha maji hayapatikani umbali unaozidi mita 400.

**Kwa kuanzia huu mtambo tunaupeleka katika Kijiji cha Itumbi kilichoko Kata ya Matundasi wilayani Chunya ambako tunakwenda kuwachimbia wale wachimbaji wa madini visima ili kutimiza ahadi ya waziri wangu.**

"Kwa kuanzia huu mtambo tunaupeleka katika Kijiji cha Itumbi kilichoko Kata ya Matundasi wilayani Chunya ambako tunakwenda kuwachimbia wale wachimbaji wa madini visima ili kutimiza ahadi ya waziri wangu," alisema Mahundi.

Alisema serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maji katika maeneo mbalimbali ya nchi na kwamba kwa Mkoa wa Mbeya mradi mkubwa unaotekelezwa ni wa chanzo cha maji cha Mto Kiwira.

Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Hance Patrick, alisema mtambo huo utasaidia kuongeza upatikanaji wa maji vijijini katika mkoa huo kutoka asilimia 63 za sasa mpaka asilimia 85 ifikapo mwaka 2025.

Alisema mitambo hiyo imeshaandaliwa utaratibu wa kusafirishwa kwenda kuzinduliwa Itumbi kwa kuanza kuwachimbia wachimbaji wa madini visima.

Aliihakikishia serikali kwamba watasimamia mitambo hiyo kwa weledi ili kuhakikisha inatumika kwa kazi iliyopangwa na wananchi wanatatuliwa kero ya maji.

"Sasa hivi tukishamaliza hapa mitambo hii inaanza kuondoka hapa kwenda wilayani Chunya kwa ajili ya kuzinduliwa, baada ya hapo itakuwa inazunguka katika maeneo mbalimbali ya mkoa huu kwa utaratibu tutakaouweka," alisema Mhandisi Patrick.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Dk. Stephen Mwakajumilo, aliwataka viongozi wa mkoa huo kupanga ratiba ya mitambo hiyo kufanya kazi kwenye wilaya zote ili kuondoa upendeleo wa baadhi ya wilaya.

Pia aliwataka wasimamizi wa mitambo hiyo kuhakikisha wanaitunza ili itumike kwa muda mrefu na kutatua kero ambayo inakusudiwa kutatuliwa na serikali.

Akipokea mtambo huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera aliishukuru serikali kwa kununua mitambo hiyo akieleza kuwa itasaidia kuwasogezea huduma wananchi kama ambavyo wamekuwa wakihitaji.

Alisema alimwomba Waziri wa Maji, Juma Aweso, kuwachimbia visima wananchi wa Kijiji cha Itumbi ambacho kina wachimbaji wengi na hawana huduma hiyo.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizindua moja ya magari yaliyo kwenye seti ya mtambo wa kuchorongea visima baada ya kukabidhiwa na Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi (hayupo pichani), jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Madiwani watakiwa kusimamia usafi kuepuka magonjwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wametakiwa kusimamia usafi kwenye maeneo yao ili kuepuka magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu na magonjwa ya kuhara.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alitoa kauli hiyo juzi kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ya Mbeya (DCC) kilichokuwa na lengo la kujadili mgawanyo wa Jimbo la Mbeya Mjini pamoja na mgawanyo wa halmashauri.

Dk. Tulia alisema wapo baadhi ya madiwani wamechukua tenda za kufanya usafi kwenye kata zao lakini hawafanyi vizuri jambo ambalo linasababisha maeneo hayo yaendelee kuwa machafu.

Alisema kitendo cha madiwani hao kushika tenda hizo kinaweza kikasababisha mgongano wa masilahi na kusababisha maeneo hayo kuingiwa na migogoro isiyokuwa na sababu.

"Madiwani nawaomba msimamie vizuri suala la usafi wa mazingira kwenye maeneo yao maana hii inaweza ikasababisha mgogoro wa masilahi, wengi mmechukua tenda za kufanya usafi na tunajua," alisema Dk. Tulia.

Meya wa Jiji la Mbeya, Sheikh DorMohamed Issa, alisema kwa sasa wanaendelea kuboresha mfumo mpya wa ufanyaji usafi baada ya kubadili ule wa awali ambao ulikuwa unasimamiwa na halmashauri moja kwa moja.

Alisema kwa sasa suala la usafi wamekasimisha madaraka kwa viongozi wa kata ambao wamepewa utaratibu wa kuajiri kampuni ya kufanya usafi.

## Maofisa Tanzania, Malawi wakutana kujadili hali ya usalama mpakani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VYOMBO vya ulinzi na usalama vya Tanzania na Malawi kutoka mikoa ya mpakani, vimekutana jijini Mbeya kujadili hali ya usalama wa nchi hizo na namna ya kukomesha biashara haramu zinazofanyika maeneo ya mpakani.

Mkutano huo pia unalenga mataifa hayo kuchukua tahadhari ya pamoja dhidi ya matukio ya ugaidi yanayoweza kuhatarisha amani kwenye maeneo hayo.

Akifungua mkutano huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema mkutano huo ni muhimu kutokana na ongezeko la matukio ya uhalifu ambayo yameanza kukithiri maeneo ya mpakani.

Homera alisema katika siku za hivi karibuni kumekuwapo na ongezeko la matukio ya uhalifu unaovuka mipaka, kama vile biashara ya binadamu, magendo na mauaji ya watu wasiokuwa na hatia.

"Kumekuwapo pia matukio ya wizi wa vyombo vya moto kama vile pikipiki ambazo zinaibwa Tanzania na kwenda kuuzwa Malawi au zinaibwa Malawi zinakuja kuuzwa Tanzania, mbaya zaidi wakati mwingine wezi hao wanalazimika kuwaua wananchi wetu ili waweze kupora vyombo hivyo, tunahitaji kushirikiana ili kukomesha uhalifu huu," alisema Homera.

Alisema ushirikiano huo pia utasaidia nchi hizo kudhibiti biashara ya magendo ambayo inazikosesha nchi zote mbili mapato kutokana na wanaofanya biashara ya magendo kutolipa kodi.

Mkuu wa Msafara wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya Tanzania, ambavyo vimeshiriki mkutano huo, Brigedia Jenerali Charles Feruz, alisema lengo la mkutano huo ni kujadili namna ya kukabiliana na makosa yanayovuka mpaka ambayo yameanza kukithiri katika nchi hizo.

Alisema biashara haramu ya binadamu, ugaidi na magendo ni miongoni mwa mambo muhimu yatakayotawala mjadala kwenye mkutano huo na kuyatafutia ufumbuzi wa pamoja katika mpaka wa nchi hizo.



# Dk. Mwinyi aipongeza Sweden kusaidia uchumi, maendeleo

Na Mwandishi Wetu

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi ameishukuru Serikali ya Sweden kwa kuiunga mkono Serikali ya Zanzibar kwa kuisaidia kwenye masuala mbalimbali ya uchumi na maendeleo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana Ikulu, Zanzibar wakati akizungumza na Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Charlota Ozaki Macias.

Alisema hatua ya Serikali ya Sweden kuisaidia Zanzibar kwenye sekta za elimu na kilimo cha baharini, ikiwamo kilimo cha mwani na kuwasaidia kinamama kisiwani Pemba kwenye kilimo cha ufugaji samaki ni kuendeleza jitihada za serikali yake katika kutekeleza adhima ya kuongeza ajira kwa wananchi hasa kuwainua wanawake kiuchumi.

**Shirika la Umeme Zanzibar, (ZECO) liko tayari kwa hatua hiyo kuanza wakati wowote na ni jambo la faraja endapo Zanzibar ikipata kujitegemea kwenye uzalishaji wa nishati ya umeme.**

Dk. Mwinyi pia aliiomba Serikali ya Sweden kupitia ubalozi wake kuisaidia Zanzibar kwenye sekta ya nishati, ambapo kwa sasa Zanzibar inadhamira ya kuzalisha umeme wake.

Alisema Shirika la Umeme Zanzibar, (ZECO) liko tayari kwa hatua hiyo kuanza wakati wowote na ni jambo la faraja endapo Zanzibar ikipata kujitegemea kwenye uzalishaji wa nishati ya umeme.



Kuhusu dhamira yake ya kuimarisha uchumi wa buluu, Rais Dk. Mwinyi aliishukuru serikali ya Sweden kwa kuendeleza jitihada zao kwenye sekta hiyo.

Alisema ukulima wa mwani kwa Zanzibar ni shughuli inayofanywa na kinamama wengi hivyo alipongeza Serikali ya Sweden kwa kuwawezesha wanawake hao.

Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Charlota Ozaki Macias, alisema Serikali ya Sweden inafanyakazi kwa karibu zaidi na Serikali ya Zanzibar katika nyanja mbalimbali ikiwamo elimu.

Hivyo, alimwahidi Rais Mwinyi kwamba Serikali ya Sweden na Zanzibar wataendeleza ushirikiano uliopo katika kukuza sekta ya nishati na uwekezaji na kumwahidi kwamba wapo tayari kwa hatua za upembuzi yakinifu kwenye masuala ya uwekezaji.

## Timu ya wataalamu kuundwa kuchunguza athari tetemeko

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imepanga kuunda timu ya pamoja na wataalamu kutoka Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kwa lengo la kufanya tathmini ya athari zilizojitokeza kutokana na tetemeko la ardhi lililotokea Februari 8, mwaka huu kisiwani Pemba.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na wizara hiyo na kusainiwa na Katibu Mkuu wake, Joseph Kilangi, imesema kamati hiyo inaundwa kwa kushirikiana na wataalamu wa jiolojia waliopo Zanzibar pamoja na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

Alisema mbali na kuangalia tathmini hiyo lakini timu hiyo inaundwa kuangalia mienendo ya mitikisiko ardhini kwa kipindi cha miezi sita nyuma kutoka Agosti 22 hadi Januari 2023 na uwezekano wa kutokea matetemeko mingine.

Alisema tume hiyo pia itaandaa mwongozo wa namna ya kujikinga na matetemeko ardhini na kuangalia majanga mengine ya kiasili ya kijiolojia baada ya tetemeko hilo.

Hata hivyo alisema uchunguzi wa kina wa tetemeko lililotokea unatarajiwa kukamilika kipindi cha wiki mbili ambapo wizara itaweka wazi ripoti ya matokeo hayo kwa wananchi.

Tetemeko hilo la ardhi lenye ukubwa wa 4.7 katika kipimo cha Richter lililotokea Februari 8, mwaka huu, ambapo kwa mujibu wa Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Maadini Tanzania (GST) limetokea magharibi mwa mwambao wa kisiwa cha Pemba umbali wa kilomita 33 katika longitude 39 30'00" na latitude 4 55'11".

**Uchunguzi wa kina wa tetemeko lililotokea unatarajiwa kukamilika kipindi cha wiki mbili ambapo wizara itaweka wazi ripoti ya matokeo hayo kwa wananchi.**



Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Muhammed Said (katikati), akizungumza na Naibu Waziri wa Mambo ya Kale na Utalii wa Oman, Ibrahim Al-harous, baada ya kutiliana saini nchini Oman juzi, makubaliano ya ujenzi wa jengo la Beit-al-Ajaib Zanzibar utakaogharimu dola za kimarekani milioni 21 na kujengwa na serikali ya Oman. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazabuni waliopewa tenda watakiwa kuzingatia masharti

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, imewataka wazabuni waliopewa kazi ya kusambaza vifaa vya maabara za Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS), kuzingatia masharti yaliyomo katika mkataba ili kufanikisha malengo yaliyowekwa.

Akizungumza jana katika hafla ya utiaji saini wa mkataba wa usambazaji wa vifaa hivyo kati ya wizara hiyo na Kampuni ya Steps Holdings Ltd na Lab Equip Ltd, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Aboud Hassan Mwinyi, alisema hatua hiyo itaongeza kasi ya utekelezaji wa mradi wa uhuishaji uchumi jumuishi Zanzibar.

Alisema kuwa hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi huo na imelenga kuiongezea uwezo wa kiutendaji ZBS kwa kuipatia vifaa vya maabara itakayoweza kupima bidhaa za ujenzi, hivyo kuongeza ufanisi katika sekta hiyo.

"Katika mradi huu kuna kipengele za ujenzi wa miradi ya serikali, sekta binafsi na hata makazi ya wananchi, hivyo kuwapo kwa vifaa na maabara zitakazoweza kupima na kutoa matokeo katika muda mfupi, kutachochea kasi ya utekelezaji wake lakini uhakika wa miradi," alisema Dk.Mwinyi.

Aidha, aliitaka ZBS kuhakikisha inavitumia kikamilifu na kuvitunza vifaa hivyo ili vitumike kwa muda mrefu na kutoa matokeo yanayotarajiwa ya kuimarisha uchumi na kudhibiti bidhaa zisizo na ubora nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa ZBS, Yusuph Majid Nassor, aliishukuru serikali kwa kuipatia vifaa vya maabara za vifaa vya ujenzi akisema itaiongezea uwezo taasisi hiyo kudhibiti bidhaa zisizo na viwango.

Alisema katika kipindi cha siku 60, vifaa hivyo vinatakiwa viwe vimekabidhiwa kwao na kwamba wamekamilisha maandalizi ya msingi ili vitakapofika visichukue muda mrefu kabla ya kuanza kutumika.

Majid alieleza kuwa vifaa hivyo pia vitapunguza gharama za uchunguzi wa ubora wa bidhaa za ujenzi zikiwamo mabati, nondo, kokoto na lami ambazo kwa sasa inabidi visafirishwe nje ya Zanzibar ili kupima ubora wake.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Kampuni ya Steps Holdings Ltd, Vincent Sixmund, aliahidi kuzingatia masharti ya mkataba na kuhakikisha vifaa atakavyowasilisha vinakua na ubora.

Aidha, alipongeza serikali kwa kusimamia vyema mradi huo na kutoa fursa kwa kampuni ya ndani kusambaza vifaa hivyo jambo linaloongeza uimara wa uchumi wa taifa.

Akizungumzia mradi wa BIG Z, Mkurugenzi Sera, Mipango na Utafiti, Wizara ya Fedha na Mipango, Mohamed Hassan Khamis, alisema kuwa mradi huo umelenga kushajihisha uchumi jumuishi ikiwamo ujenzi wa miundombinu na majengo mbali mbali.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ONESMO NYAKURA NDEGI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE** yenye usajili namba: **T285 DHM, CHASSIS NAMBA: LH1230001285** na **ENGINE NAMBA:3L0001285** na kadi ya gari aina ya **NISSAN VANNETTE** yenye usajili namba: **T636 DFU, CHASSIS NAMBA: SK82VN103784** na ENGINE NAMBA:F80263784. KWA YEYOTE ATAKAEZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. Polisi taarifa: **DAR/CEN/RB/61917/2013**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LILIAN ONESMO NDEGI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba: T**368 DAR, CHASSIS NAMBA: AZR60007225232** na ENGINE NAMBA: **IAZA234** . Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa: **DAR/CEN/RB/61970/2013**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**APPOLINARI MINJA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 652 CSC – SUZUKI CARRY.** Chassis namba **DD51T537092.** Engine namba **F6912547**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/494819/2022**.

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**HEKIMA ELIA MALILA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC. 931** CAD.YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/61647/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



117264602

**SAIDA HAFIDHI CHANDE** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria yenye passport namba **TAE374609** iliyotolewa DAR ES SALAAM PCO mwaka 2020. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/KIL/RB/61510/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**
**MAOMBI NAMBA 41 YA 2022**

**MIKALI ABDUEL MSUYA**
**YOSEA HERMAN MSUYA.............WALETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**MAENDELEO BANK TANZANIA PLC**
**BEST GROUP (T) LIMITED**
**ELIZABETH DORIS MASI............WAJIBU MAOMBI**

**WITO WA KUITWA SHAURINI KWA**
**BEST GROUP (T) LIMITED** Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Morogoro terehe **08/03/2023** mbele ya mwenyekiti M.Khasim wewe mwenyewe binafsi au utume mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa **MKONO** wangu na **MUHURI** wa Baraza leo tarehe **13** mwezi Februari **2023**


**OFISI ZA MATANGAZO**

**Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042,**

**Dar es Salaam. Mobile: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**Website: www.ippmedia.com**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu (katikati), akikata utepe kukabidhi madawati 150 yaliyotolewa na Benki ya Stanbic chini ya mpango wake wa Madawati Initiative, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya shule mbili za sekondari za Gerezani na Dar es Salaam. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi wa Benki hiyo, Omari Mtiga (kushoto) na Diwani wa Gerezani, Fatuma Abubakari Ally, Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Dar es Salaam, Hossain Njau na viongozi wa serikali za mitaa, wanafunzi na walimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT yatia neno mchakato kufumua Sheria ya Habari

**Na Mwandishi Wetu**

ADO Shaibu, Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo amesema serikali imeanza na mguu mzuri kuelekea mabadiliko ya Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016.

Kiongozi huyo alitoa kauli hiyo jana ikiwa ni siku tano baada ya serikali kuwasilisha mapendekezo ya marekebisho ya vipengele vya sheria hiyo bungeni.

Alisema hatua ya serikali kuwasilisha mapendekezo hayo yaliyobeba sehemu ya mabadiliko ya sheria hiyo, inaakisi kuelekea katika uhuru wa kweli wa habari nchini.

"Nimepitia muswada huo kwa haraka, kwa namna yake umegusa baadhi ya mambo ambayo wanahabari walikuwa wanalalamikia na kweli yalikuwa yana ukakasi mkubwa.

"Miongoni mwake ni lile la Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) kupunguziwa mamlaka ya kuhukumu vyombo vya habari, hapa unaona wazi dhamira ya kufanya vyombo vya habari kuwa huru inaonekana. Pia nimeona marekebisho kuhusu kupunguzwa kwa faini," alisema Shaibu.

Hata hivyo, Katibu Mkuu huyo alishauri wadau wa habari kuupitia muswada huo kwa makini ili kujiridhisha kwa namna ambayo vyombo vya habari vitakuwa imara zaidi ya ilivyo sasa.

"Pamoja na kwamba muswada umesomwa kwa mara ya kwanza, bado wadau wa habari wanapaswa kuupitia kwa umakini zaidi kipengele kwa kipengele ili kujiridhisha.

"Jambo hili likipita, itachukua muda mrefu kufanya marekebisho mengine. Hii ni fursa ambayo serikali imewapa na wanapaswa kuitumia vizuri," alisisitiza.

Pia alishauri wadau wa habari kukutana na wabunge kwa nyakati tofauti kwa ajili ya kufafanua zaidi kile wanachokihitaji kwa kuwa ndio watunga sheria.

"Ninashauru wadau wa habari wajitahidi kuwaeleza wabunge dhamira halisi na nini thamani ya kuwa na vyombo vya habari huru.

"Ninasema hivyo kwa kuwa wabunge ndio watunga sheria, wanapokuwa na ufahamu mkubwa kuhusu mabadiliko haya, wanaweza kusaidia kwa kiwango kikubwa kutunga sheria zitakazoleta uhuru wa habari kwa muda mrefu," alisema.

Akizungumzia mchakato huo, Shaibu alisema serikali yoyote dunia haiwezi kutamba kuwa inaenzi demokrasia huku ikiminya uhuru wa vyombo vya habari.

"Haiwezekani kuwa na demokrasia kama hakuna uhuru wa habari. Hivi vitu viwili vinategemeana, mahali ambapo demokrasia inastawi, tunatarajia uhuru wa habari nao utakuwa umeshamiri na sehemu ambayo uhuru wa habari umeshamiri, demokrasia nayo inashamiri.

"Uhuru wa vyombo vya habari na maendeleo ya taifa ni chanda na pete. Nchi ikiendeshwa gizani, nchi ikiendeshwa bila uwazi, nchi ikikosa uhuru wa habari, nchi hiyo haiwezi kuwa na maendeleo ya kweli," alisema.

Shaibu alisema jambo ambalo baadhi ya watawala hasa wa Afrika hawalielewi, wanadhani kuwa habari ni adui kwao na ni adui kwa serikali.

"Utaona katika nchi nyingi za Afrika jitihada zimekuwa zikifanywa na serikali kuzuia uhuru wa habari, serikali zimekuwa zikiweka sheria kuhakikisha vyombo vya habari vimekuwa havifurukuti.

"Ukweli ni kwamba uhuru wa habari unasaidia sana serikali kutekeleza wajibu wake, unalisaidia sana taifa kusonga mbele," alifafanua.

Deodatus Balile, Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) alisema tayari muswada huo ameupitia na kwamba yeye na wadau wengine wa habari wanapanga kukutana ili kuuchambua kwa pamoja ili kuwa na kauli moja.

# Serikali yamulika maeneo matatu kuvutia wawekezaji

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imetaja maeneo matatu iliyoboresha ili kuwavutia wawekezaji kutoka nje, yakiwamo marekebisho ya sheria ya uwekezaji na kuondoa utitiri wa kodi.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alibainisha hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati wa mkutano wa ngazi ya juu wa majadiliano ya kimkakati kati ya serikali na washirika wa maendeleo.

Dk. Nchemba alisema serikali inatambua umuhimu wa wawekezaji wa ndani na nje, hivyo imeshafanya jitihada za kuboresha mazingira kuwa rafiki na kuwavutia.

"Tumefanya marekebisho katika sheria ya uwekezaji, tumechukua hatua za kikodi kwa kuondoa utitiri wa kodi, pia tumeingia mikataba ya soko la bidhaa. Kwa mfano, Rais Samia alipokwenda China, aliingia makubaliano ya biashara ya samaki.

"Miaka kadhaa iliyopita kulikuwa na malalamiko ya wafanyabiashara kuhusu utitiri wa kodi, Rais Samia alipoingia madarakani alifuta tozo na kodi zaidi ya 114, katika sekta za uzalishaji pia alifuta tozo na kodi mbalimbali ambazo zinahusisha sekta hizo, lengo ni kuzifanya sekta hizo zivutie," alisema.

Waziri huyo alisema serikali imetia saini mikataba ya makubaliano na nchi mbalimbali kwa ajili ya soko la bidhaa.

Alisema mojawapo ya mambo yaliyokuwa yanavunja moyo serikali kwenye sekta za uzalishaji ni bidhaa zinazozalishwa kukosa soko.

"Tulitia saini makubaliano kwenye ziara ya Rais Samia alipokwenda China kuhusu samaki, parachichi, kwenye ziara aliyofanya Ulaya makubaliano yalisainiwa katika nafaka ambapo mchele wa Tanzania unauzwa hadi Ubelgiji, pia tulitiliana saini na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) na nchi nyingine zinazotuzunguka," alisema.

Alisema jitihada hizo za serikali zinalenga kuchochea uzalishaji na kuongeza pato la wazalishaji.

Kuhusu uzalishaji katika kilimo, mifugo na uvuvi, waziri huyo alisema lengo la serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 mchango wa sekta hizo uwe umezidi asilimia 10 ili pato la taifa linapopanda na pato la mtu mmoja mmoja nalo lipande.

Kadhalika, aliwataka washirika wa maendeleo kuhakikisha wanaoanisha jitihada zao za maendeleo ili ziendane na za serikali.

Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salim, alisema mkutano huo unaipa fursa Zanzibar kuzungumza na wadau hao wa maendeleo katika uchumi wa buluu.

Alisema asilimia 40 ya wananchi wa Zanzibar wanategemea shughuli za uvuvi kuendesha maisha yao.


## FURSA YA BIASHARA YA UWAKALA WA BIMA

Biashara ya bima nchini Tanzania inaelekea kukua kwa kasi katika wakati ujao. Ili kutumia fursa hii, moja kati ya kampuni ya bima inayokua kwa kasi zaidi, yenye jina dhabiti na inayoaminika nchini inawaalika wamiliki wa biashara mbalimbali, taasisi na watu binafsi walio na ushawishi na mtandao mpana kutuma maombi ya leseni ya wakala.

Kwa kawaida, mawakala hupata kamisheni na bonasi kutokana na biashara za bima wanazopata. Kampuni ya bima itatoa mafunzo na usaidizi wote katika michakato ya usajili na maendeleo ya biashara.

Maombi ya uwakala yaambatane na taarifa zifuatazo: -

a) Jina la kampuni na wasifu wa biashara

b) Mahali ofisi yako ilipo
- Barua pepe
- Nambari ya simu ya mkononi/Nambari ya simu ya Biashara

c) Jina la mtu wa mawasiliano na anwani atakayekua anashughulikia biashara ya uwakala.

Makampuni au watu binafsi wanaovutiwa wanaweza kutuma maombi ya wakala wa bima kupitia barua pepe yetu shaheem**consultancy@gmail.com**

217281002

# YANGA PRINCESS KIBARUANI LEO, OPA MCHEZAJI BORA JANUARI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI timu ya soka ya wanawake ya Klabu ya Yanga, Yanga Princess, inamaliza mzunguko wake wa kwanza wa Ligi Kuu leo, itakapojitupa Uwanja wa Uhuru, Dar es Saalam kucheza dhidi ya Amani Queens kutoka mkoani Lindi, straika wa Simba Queens na Timu ya Taifa ya Tanzania, Twiga Queens, Opa Clement, amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa Januari.

Itakuwa ni mechi muhimu kwa Yanga Princess ambayo msimu huu imedhamiria kutwaa ubingwa kwa kusajili wachezaji wengi kutoka nje ya nchi ambao wameibadilisha kwa kiasi kikubwa na kuiwezesha kuvuna pointi 17 mpaka sasa.

Kwenye mechi ya mwisho iliyocheza Februari 7, mwaka huu kwenye uwanja huo huo, iliachia kipigo cha mabao 5-0 dhidi ya The Tigers Queens ya Arusha, ikiwa ni 'hat-trick' ya straika wa kimataifa wa Nigeria, Nkor Blessing, huku Mnigeria mwenzake Chioma Wogu akifunga bao moja na lingine likiwekwa nyavuni na Nadege Atanhloueto raia wa Benin.

Kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Baobab itamaliza mzunguko wake wa kwanza wa ligi dhidi ya Alliance Girls, huku The Tigers Queens ikiikaribisha Fountain Gate Princess kwenye Uwanja wa Black Rhino, Karatu, Arusha.

Mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo utamalizika rasmi kesho kwenye Uwanja wa Meja Jenerali, Isamuhyo uliopo Mbweni, Dar es Salaam, timu tishio ya Maafande wa JKT Queens watakapocheza dhidi ya Mkwawa Queens kutoka Iringa.

Wakati huo huo, Opa amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi Januari kwenye ligi hiyo. Taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka nchini (TFF), inasema Opa ambaye ndiye anayeongoza mpaka sasa kwa mabao, akipachika mabao tisa, amechaguliwa baada ya kufanya vema mwezi huo.




Mkurugenzi wa Kemon Sports Agency na Promota wa Ngumi, Saadah Salum (wa pili kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mashindano ya ngumi yanayotarajiwa kufanyika baadaye Februari 24, mwaka huu. Kulia ni bondia, Oscar Richard, Mdau wa michezo, Jackson Ngumba (wa pili kushoto) na bondia Adam Mbega. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mabondia 20 wapima afya kuvaana Februari

**Na Saada Akida**

MABONDIA wa ngumi za kulipwa nchini, Tony Rashid na Oscar Richard, jana wameongoza kundi la mabondia kupima afya zao tayari kwa pambano linalotarajiwa kupigwa Februari 24, mwaka huu, kwenye Ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

Katika pambano hilo la Ubingwa wa Afrika (ABU), utawaniwa na Seleman Kidunda dhidi ya Patrick Mukala huku Tony Rashid akipanda pia ulingoni kutetea mkanda wake wa Ubingwa wa ABU dhidi ya Sabelo Ngabinyana raia wa Afrika Kusini.

Kuelekea mpambano huo, ambao utakuwa na mikanda mitatu ya Ubingwa Afrika na Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), mapambano 10 yatafanyika na jana jumla ya mabondia 20 walipima afya zao.

Mabondia hao waliopima afya ni Selema Kidunda na Patric Mukala, Oscar Duke na mpinzani wake, Adam Mbega, Emmanuel Mwakyembe na Francis Miyeyusho.

Wengine ni Mbaraka Mtangebandu, Hamza Mchanjo, Omari Omari, Muhsin Kizota, Alex Kachelewa, Adam Mrisho, Mwinyi Mzengela, Ajemi Amani, Abdul Kubila, Msabaha Salum, Ahmed Pelembela, Iddi Pazi, Halima Bandola na Flora Machela.

Promota wa pambano hilo, Saadah Salum, alisema wamekamilisha zoezi la kwanza kwa upimaji afya za mabondia kuelekea pambano hilo la Februari 24, mwaka huu.

"Tayari leo (jana), tumekamilisha sehemu ya kwanza ya maandalizi kwa kupima afya za mabondia wote kutokana na kanuni na sheria za mchezo wa ngumi za kulipwa hapa nchini," alisema Saadah.

# Kocha Medo aomba radhi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Dodoma Jiji FC, Melis Medo, ameomba radhi kwa waamuzi wa mchezo wa mpira wa miguu na wadau wote kwa ujumla kutokana na kitendo alichofanya cha kumpokonya kadi ya njano mwamuzi wa kati na kumuonyesha kadi hiyo mwamuzi wa akiba kwenye mechi kati ya timu yake dhidi ya Mtibwa Sugar iliyochezwa Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

Medo alifanya kituko hicho Jumamosi iliyopita ukiwa ni mchezo namba 185 wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Mtibwa Sugar ikishinda mabao 2-1.

Baada ya kufanya hivyo, mwamuzi aliamua kumtandika kadi nyekundu na kulazimika kutoka nje ya uwanja, akiiacha timu yake ikiongozwa na Kocha Msaidizi, Kassim Liogope.

"Ukiacha mbali kuwa kitendo kile ni kinyume na kanuni za ligi, lakini hakikuwa cha kiungwana. Nimekosea, naomba radhi kwa wamuzi wa mchezo ule, uongozi wa Bodi ya Ligi, Uongozi wa Dodoma Jiji na wadau wote wa soka," alisema kocha huyo.

# Kopa asema jimbo lake liko wazi

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI nyota wa Muziki wa Taarab, Khadija Kopa maarufu 'Malkia wa Mipasho Afrika Mashariki', amesema yuko tayari kuolewa, lakini ameweka masharti kwa ambaye yuko tayari kumuoa.

Alisema tangu Juni mwaka 2013, mume wake aliyekuwa akiitwa Jaffari Ally, alipofariki dunia, anaishi kivyake na kwamba kama yupo muoaji, ni lazima awe ni wa umri wa kuanzia miaka 50 na kuendelea.

"Mimi jimbo liko wazi, tangu mume wangu afariki dunia, niko peke yangu. Mtu wa kunioa akija, lazima awe na umri mkubwa kuanzia zaidi ya miaka 50 na kwenda juu," alisema Kopa.

Msanii huyo alisema hayo alipokuwa akihojiwa na EATV na kufafanua kuwa muoaji pia anayemtaka awe anajiweza kimaisha amtunze, na kwamba watasaidiana, shida zake mumewe azijue, awe ni mtu wa dini.

"Unavyoniona situmii pombe, sivuti bangi, sivuti sigara, yaani situmii ulabu wowote," hivyo nikipata mume anayeendana na mfumo wangu wa maisha, itakuwa vizuri sana," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHELSEA KUMNUNUA FELIX

KLABU ya Atletico Madrid huenda ikakubali kumuuza mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 23, kwa Chelsea kwa euro milioni 100 msimu wa majira ya joto. Klabu hiyo ya LaLiga ilikuwa ikihitaji kati ya euro milioni 130. ***(Relevo)***

### PULISIC KWENDA ATLETICO

KIUNGO wa kati wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic, huenda akaelekea kinyume upande mwingine na Joao Felix, huku Atletico Madrid wakifikiria dau lililopunguzwa la mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ambaye alisajiliwa na 'The Blues' hao mwaka 2019 kwa pauni milioni 57.6. ***(Fichajes)***

### RICHARLISON KUMRITHI BENZEMA

REAL Madrid inamfuatilia mshambuliaji wa Juventus, Mserbia Dusan Vlahovic, mwenye umri wa miaka 23, na nyota wa Tottenham Hotspur, Richarlison (25), kama mbadala wa muda mrefu wa mshambuliaji wa zamani wa kimataifa wa Ufaransa, Karim Benzema, 35. ***(ESPN)***

### NEYMRA SOKONI PSG

KLABU ya Paris St-Germain huenda wakamweka sokoni mshambuliaji wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 31 - ambaye walimsajili kwa kima cha euro milioni 222 kutoka Barcelona mnamo 2017 - kwenye orodha ya uhamisho wa majira ya joto. ***(Foot Mercatoa)***

### OFA YA UNITED WIKI HII

MAMLAKA ya Uwekezaji ya Qatar itatoa ofa rasmi ya karibu pauni bilioni tano, kuinunua Manchester United ifikapo mwishoni mwa wiki hii. ***(Telegraph)***

### BAYERN YAJITOA KWA THURAM

KLABU ya Bayern Munich imejiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Marcus Thuram, mwenye umri wa miaka 25, kutoka Borussia Monchengladbach, lakini Inter Milan na AC Milan nazo zinamwania. ***(Sempre Inter)***

### KANE ANYATIWA BAYERN

KLABU Bayern Munich imeelekeza darubini yake kwa nahodha wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29, huku Randal Kolo Muani mwenye miaka 24 wa Eintracht Frankfurt akiorodheshwa kuwa mbadala. ***(La Gazzetta dello Sport via Sempre Inter)***

### ROQUE ATAJWA ARSENAL

MSHAMBULIAJI wa Athletico Paranaense, Vitor Roque mwenye umri wa miaka 17, ambaye hivi karibuni aliisaidia Brazil kushinda taji la Amerika Kusini la wachezaji wa chini ya miaka 20, anaongoza orodha fupi ya uhamisho wa Arsenal majira ya joto. ***(AS)***

### SERGI KUBAKI BARCA

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Sergi Roberto mwenye umri wa miaka 31, amekubali masharti ya kuongeza mkataba wake na Barcelona ambao utamweka katika klabu hiyo hadi Juni 2024. ***(Fabrizio Romano).***

### MARSCH NA SOUTHAMPTON

KLABU ya Southampton imefanya mazungumzo na kocha Mmarekani mwenye umri wa miaka 49, Jesse Marsch - aliyetimuliwa na Leeds United wiki iliyopita kuchukua nafasi ya Nathan Jones. ***(TalkSport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR SASA ALITAKA KOMBE LA DUNIA 2026

**Nitaenda mwaka baada ya mwaka na tutaona, bila shaka, nina ndoto kubwa ya kushinda...**

**PARIS,Ufaransa**

NEYMAR amedokeza kuwa bado anaweza kucheza Kombe la Dunia la 2026, akifichua kwamba "ndoto kubwa" bado inawaka kwake ili kulinyakua kombe hilo.

Mchezaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 31, alisema katika kuelekea michuano ya Kombe la Dunia mwaka jana kwamba inaweza kuwa ya mwisho kwake, huku akiachwa akiwa amehuzunishwa na kuondolewa kwa nchi yake na Croatia katika robo fainali.

Baada ya Brazil kutolewa katika Kombe la Dunia, Neymar hakutoa hakikisho lolote kuhusu mustakabali wake wa kimataifa.

Miezi miwili baadaye sasa Neymar anaonekana kusema kwamba mlango haujafungwa katika maisha yake ya soka ya Brazil hadi Kombe la Dunia 2026.

"Nitaenda mwaka baada ya mwaka na tutaona," alisema Neymar akiiambia TNT Sports.

"Bila shaka, nina ndoto kubwa sana, ya kushinda Kombe la Dunia."

Neymar aliongeza kwamba alitiwa moyo na mchezaji mwenzake wa Paris Saint-Germain, Lionel Messi, akiwa na Argentina nchini Qatar.

"Leo daima amekuwa msukumo kwangu," alisema. "Kila mara alinisaidia na kunitia moyo. Ni wazi, kumwona akishinda akiwa na miaka 35, nafikiri juu yake pia."

Neymar atakuwa na umri wa miaka 34 wakati Kombe la Dunia la 2026 litakapoanza nchini Marekani, Mexico na Canada.

Fowadi huyo alikuwa sehemu ya kikosi cha Brazil cha Kombe la Dunia la 2014, 2018 na 2022, akishinda Kiatu cha Shaba na kutajwa katika 11 bora ya kikosi cha Fifa cha mwaka 2014.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,077,4

JACKPOT MECHI WIKI HII

TAREHE: 15,16 NA 17 FEBRUARI 2023

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 15/02/23 | 20:00 | Omonia Nicosia vs Apoel Nicosia | 2.55 | 3.16 | 2.55 |
| 02. 15/02/23 | 22:30 | Arsenal vs Manchester City | 2.71 | 3.24 | 2.48 |
| 03. 15/02/23 | 22:45 | Motherwell vs St Mirren | 2.36 | 3.23 | 2.93 |
| 04. 15/02/23 | 22:45 | Preston vs Luton Town | 2.53 | 3.13 | 2.73 |
| 05. 15/02/23 | 23:00 | Borussia Dortmund vs Chelsea | 2.37 | 3.37 | 2.77 |
| 06. 16/02/23 | 06:05 | Club Necaxa vs UNAM Pumas | 2.45 | 3.35 | 2.71 |
| 07. 16/02/23 | 20:45 | RB Salzburg vs Roma | 2.73 | 3.23 | 2.53 |
| 08. 16/02/23 | 20:45 | Sporting Braga vs Fiorentina | 2.43 | 3.39 | 2.74 |
| 09. 16/02/23 | 23:00 | Sevilla FC vs PSV Eindhoven | 2.24 | 3.39 | 3.05 |
| 10. 16/02/23 | 23:00 | Sheriff Tiraspol vs Partizan | 2.50 | 3.20 | 2.80 |
| 11. 17/02/23 | 00:00 | Mirassol SP vs Ituano SP | 2.68 | 2.89 | 2.63 |
| 12. 17/02/23 | 03:30 | Corinthians vs Palmeiras | 3.00 | 2.75 | 2.24 |
| 13. 17/02/23 | 11:45 | Western United vs Wellington Phoenix | 2.70 | 3.23 | 2.53 |

BREAKING NEWS

SUPA JACKPOT YA MECHI - 13

TZS. 248,672,790

IMEPATA MSHINDI

SportPesa


SPORTPESA.CO.TZ

PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: LIVERPOOL SASA IMEAMKA



**LIVERPOOL, England**

JURGEN Klopp anahisi kuwa Liverpool ilituma "ujumbe" katika ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Everton ambao ulitoa "ahueni kubwa" kwao.

'Wekundu' hao juzi, Jumatatu walipata ushindi wao wa kwanza wa Ligi Kuu tangu kuanza kwa mwaka huu na kuwafanya majirani wao kuwa kwenye hatari ya kushushwa.

Mohamed Salah alitengeneza pasi nzuri na Darwin Nunez, na kisha kufunga bao la kwanza katika kipindi cha kwanza likiwa bao lake la 18 msimu huu, akimalizia shambulizi la kushtukiza sekunde 13 baada ya James Tarkowski kugonga nguzo upande wa pili.

Bao la kwanza la Cody Gakpo la Liverpool mapema katika kipindi cha pili, liliongeza matumaini kwa Wekundu hao na kuwafanya 'Toffees' hao kupokea kichapo chao cha kwanza chini ya bosi mpya, Sean Dyche, baada ya kuanza utawala wake kwa ushindi dhidi ya vinara, Arsenal.

Klopp pia aliwaanzisha Diogo Jota na Roberto Firmino kama wachezaji wa akiba kipindi cha pili katika ushindi wake wa 250 akiwa kocha wa Liverpool, huku Virgil van Dijk akirejea kwenye benchi baada ya kuuguza jeraha la misuli ya paja.

Mjerumani huyo anatumaini kuwa timu yake sasa inaweza kuimarika kutokana na kuanza vibaya mwaka baada ya kupanda hadi nafasi ya tisa, pointi tisa nyuma ya Newcastle United iliyo nafasi ya nne kabla ya safari ya St James' Park, Jumamosi.

Klopp aliiambia BBC Sport: "Ilihisi kama sisi, ilionekana kama sisi. Matokeo yake ni ahueni kubwa. Usiku wa leo (juzi), kila mtu anaanza kuamini tena kidogo zaidi. Lazima tuendelee.

"Uchezaji ulikuwa taarifa kwetu kwamba tunaweza kufanya hivi. Ilibidi tucheze mchezo wetu na ndivyo ilivyokuwa kwa dakika 95 na ndio maana tulistahili kupata alama.

"Ili kutoka katika hali yetu, tunahitaji maonyesho kama haya. Tulikuwa na bahati wakati Tarkowski alipogonga nguzo. Darwin alipiga shuti kali. Bao la pili lilikuwa shambulio la ajabu pia. Tulikuwa na nguvu nyingi. Sijui takwimu, lakini lazima iwe, ulikuwa wa asilimia 70."

# CR7, Messi, Mbappe ndani ya FIFPro

**PARIS, Ufaransa**

CRISTIANO Ronaldo, Lionel Messi na Kylian Mbappe wote wametajwa kwenye orodha ya wachezaji 26 walioteuliwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), kama kikosi bora cha Wanaume cha Fifa 2022.

Kujumuishwa kwa Ronaldo bila shaka kulikuwa mshangao mkubwa baada ya kipindi kigumu cha nyuma cha mwaka ambapo alitemwa na Manchester United na aliachana na 'Mashetani Wekundu' hao Novemba mwaka jana.



Nyota huyo wa Ureno amekuwa akichaguliwa kwenye kikosi bora cha mwaka pamoja na Messi, kila mwaka tangu 2007, lakini atakabiliana na ushindani mkali miongoni mwa washambuliaji pamoja na Erling Haaland, Mbappe, Neymar, Robert Lewandowski na mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or, Karim Benzema.

Mwaka jana, washambuliaji wanne walitajwa katika 11 ya mwisho; Ronaldo, Haaland, Lewandowski na Messi.

Nyota wa Kombe la Dunia, Jude Bellingham na Enzo Fernandez, wametajwa kwenye orodha ya walioteuliwa kwa mara ya kwanza kwenye safu ya kiungo, pamoja na Casemiro, Kevin de Bruyne, Gavi, Luka Modric, Pedri na Federico Valverde.

Mabeki walioteuliwa ni Joao Cancelo, Virgil van Dijk, Antonio Rudiger, Thiago Silva, Alphonso Davies, Josko Gvardiol, Achraf Hakimi na Theo Hernandez.

Makipa wanaowania ni Alisson Becker, Thibaut Courtois na Emiliano Martinez.

-33,324/-

# YANGA YAIINGIZA KWENYE MTEGO TP MAZEMBE CAF

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imewataka wanachama na mashabiki wake kutoumizwa na matokeo kwa yale yaliyotokea Jumapili ilipofungwa mabao 2-0 dhidi ya Monastir nchini Tunisia, ikisema imeshaanza maandalizi ya kuwaandalia kipigo TP Mazembe mwishoni mwa wiki.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema kutokana na takwimu jinsi zilivyo, inaonyesha kuwa timu nyingi za Afrika zinashinda nyumbani, hivyo wamejiandaa vilivyo kuhakikisha inavuna pointi zote tatu kwenye ardhi ya nyumbani, akiwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo nao kujaza Uwanja wa Benjamin Mkapa kutoa sapoti kwa wachezaji ili kuwachanganya wapinzani wao.

Yanga iliwasili nchini jana mchana ikitokea Tunisia na moja kwa moja imekwenda kambini kujiandaa na mechi ya pili ya Kundi D Kombe la Shirikisho Afrika, itakayochezwa Jumapili saa 1:00 usiku, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Tunajua kila mmoja ameumizwa na matokeo, siyo matokeo ambayo tuliyatarajia, kila mmoja alikuwa amejiandaa na ushindi kwenye ardhi ya ugenini. Lakini niwaambie wanachama na mashabiki wa Yanga, tusiwe wanyonge, tusifikiri kwamba tumepoteza kitu kikubwa, ule haukuwa mchezo wa mwisho wa kundi, ulikuwa ni wa kwanza hatua hiyo.

"Ninaomba niwaambie kitu, imechezwa michezo minane kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika, mechi zote hizo, hakuna timu iliyoweza kushinda kwenye uwanja wa ugenini, ni timu tatu zimeweza kupata sare," alisema Kamwe.

Aliendelea kusema kuwa kwenye Ligi ya Mabingwa ambako zimechezwa mechi sita mpaka sasa, ni mechi moja tu ambayo timu imepoteza nyumbani.

"Ligi ya Mabingwa nako zimechezwa mechi sita, mbili hazikuchezwa kwa sababu timu zao zilikuwa kwenye michuano mingine, ukijumlisha unapata michezo 14 ya kimataifa, ni timu moja tu ambayo imepoteza nyumbani, nayo ni Zamalek ambayo ilifungwa bao 1-0 na wale CR Belouizdad ya Algeria. Kwa hiyo kuna kipigo kimoja na sare nne kwa ujumla, mechi tisa za nyumbani timu zimeshinda, tafsiri yake ni kwamba michuano hii ya Afrika, kila mtu amejiimarisha kwenye ardhi yake ya nyumbani, kwa hiyo Wanayanga tuache kuweka vichwa chini, tuangalie sasa nini tunafanya kwenye mechi ijayo dhidi ya TP Mazembe," alisema Kamwe.

IKO HIVI...



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa (katikati), akimsikiliza Katibu Mkuu wa wizara hiyo. Dk. Hassan Abbas (kushoto), walipofika kukagua viwanja vya Tanganyika Packers, Kawe jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kujenga Uwanja wa Michezo ya Ndani wa kisasa (Sports Arena). Kulia ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini, Ally Mayayi Tembele. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# RAIS SAMIA ANUNUA

INATOKA UK. 24

saa 1:00 usiku. Lakini sisi hatuangalii muda, wowote tupo tayari kupambana ili kupata ushindi. Na kama mnakumbuka tulishawahi kucheza saa nne usiku na tukapata matokeo," alisema na kuongeza:

"Waamuzi wa mchezo watatokea Cameroon na kuhusu Raja Casablanca tayari wameshawatumia taarifa kuwauliza watafika lini Tanzania lakini hadi sasa hawajajibu."

Kuhusu Sadio Kanoute alisema hatakuwapo kwenye mchezo unaokuja kutokana na kuwa na kadi tatu za njano lakini Saido Ntibazonkiza ameshapona na Peter Banda."

Ahmed alisema leo kuanzia saa tano asubuhi watafanya uzinduzi babkubwa kwenye tawi la Home Boys lililopo Tegeta kwa ajili ya hamasa ya kwenda uwanjani kuishangilia timu yao Jumamosi.

# ROBERTINHO: NI USHINDI

INATOKA UK. 24

na kesho (leo), tutazindua rasmi kampeni yetu tutaanzia Tegeta, kuhamasisha Wanasimba kuja uwanjani kwa wingi timu yao inapopambania Taifa," alisema.

Alisema taarifa kutoka kwa wapinzani wao wanatarajia kuwasili leo, lakini huwa hawatabiriki kwa sababu mara nyingi huficha.

Tayari kumekuwa na presha kwa mashabiki wa timu hizo mbili imeanza kupanda mitandaoni, kwani wakati Simba wakitamba na jezi zao zinatangaza utalii wa Tanzania, 'VISIT TANZANIA', kupitia mtandao wa kijamii wa Raja Casablanca, imetoa taarifa kuwa 'Wanakuja Serengeti', ni sehemu ya mbuga ya Tanzania na ni moja ya kivutio kikubwa cha utalii duniani.

# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII
## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/02/23 | 18:00 | Blackpool vs Stoke City | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 02. 18/02/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Birmingham City | 2.65 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 18/02/23 | 18:00 | Everton FC vs Leeds United | 2.36 | 3.30 | 2.95 |
| 04. 18/02/23 | 18:00 | Hull City vs Preston North End | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 05. 18/02/23 | 18:30 | Portimonense SC vs Maritimo Madeira | 2.29 | 3.15 | 3.15 |
| 06. 18/02/23 | 20:00 | FC Winterthur vs FC Sion | 2.45 | 3.10 | 2.44 |
| 07. 18/02/23 | 20:30 | CD Leganes vs UD Las Palmas | 2.70 | 2.90 | 2.80 |
| 08. 18/02/23 | 20:30 | Newcastle United vs Liverpool FC | 2.27 | 3.45 | 2.95 |
| 09. 18/02/23 | 20:30 | RCD Mallorca vs Villarreal CF | 3.15 | 2.95 | 2.42 |
| 10. 18/02/23 | 20:45 | FC Groningen vs FC Emmen | 2.28 | 3.20 | 3.10 |
| 11. 19/02/23 | 14:15 | SC Cambuur vs SC Heerenveen | 3.05 | 3.25 | 2.31 |
| 12. 19/02/23 | 15:00 | Motherwell FC vs Heart of Midlothian FC | 2.80 | 3.25 | 2.47 |
| 13. 19/02/23 | 16:00 | SD Huesca vs Granada CF | 3.30 | 2.95 | 2.34 |
| 14. 19/02/23 | 16:00 | Elche CF vs Espanyol Barcelona | 2.75 | 3.05 | 2.60 |
| 15. 19/02/23 | 17:00 | ESTAC Troyes vs Montpellier HSC | 2.50 | 3.20 | 2.75 |
| 16. 19/02/23 | 18:15 | Rayo Vallecano vs Sevilla FC | 2.43 | 3.00 | 3.05 |
| 17. 19/02/23 | 18:30 | Santa Clara Azores vs FC Famalicao | 2.80 | 3.15 | 2.55 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATANO - 15/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:00 | 3058 | Persepam MU vs Persita Tangerang | 2.00 | 3.26 | 3.42 |
| 14:00 | 1639 | Cagliari Youth vs Inter Youth | 2.44 | 3.42 | 2.52 |
| 14:00 | 5197 | Rajasthan United vs Gokulam Kerala FC | 2.95 | 3.06 | 2.30 |
| 15:00 | 5621 | Montenegro W vs Moldova W | 1.34 | 4.66 | 7.26 |
| 15:30 | 3466 | Al Qadisiyah vs Jeddah Club | 2.04 | 2.85 | 3.84 |
| 15:45 | 4049 | Alshoulla vs AL Sahel SC | 2.82 | 2.76 | 2.61 |
| 15:55 | 4809 | AL Hazm vs AL Qaisoma | 1.47 | 3.82 | 6.40 |
| 16:00 | 2538 | Empoli Youth vs Fiorentina Youth | 2.70 | 3.30 | 2.16 |
| 16:00 | 3324 | Estrela Amadora U23 vs Estoril Praia U23 | 2.43 | 3.42 | 2.53 |
| 16:00 | 5635 | Bologna Youth vs Roma Youth | 3.55 | 3.45 | 1.75 |
| 16:00 | 5710 | NK Zvijezda Gradacac vs Sloboda Tuzla | 3.12 | 3.64 | 1.98 |
| 16:45 | 1339 | Al Jahra vs AL Arabi | 5.07 | 3.57 | 1.61 |
| 16:45 | 5301 | AL Wakrah vs Qatar SC | 1.84 | 3.62 | 3.57 |
| 17:00 | 2681 | Bengaluru FC vs Mumbai City FC | 3.67 | 3.52 | 1.84 |
| 17:00 | 4890 | Scotland W vs Iceland W | 3.05 | 3.00 | 2.28 |
| 18:00 | 2208 | AC Milan Youth vs Sampdoria Youth | 2.21 | 3.50 | 2.49 |
| 18:00 | 2665 | Necaxa U20 vs Pumas U20 | 2.47 | 3.25 | 2.33 |
| 18:00 | 3277 | Torino Youth vs Atalanta Youth | 1.96 | 3.40 | 3.00 |
| 18:00 | 4009 | Monterrey U20 vs Queretaro U20 | 1.65 | 3.84 | 4.26 |
| 18:30 | 2766 | LYS Sassandra vs FC San Pedro | 3.30 | 2.50 | 2.27 |
| 18:30 | 5226 | Sporting Gagnoa vs Club Omnisports de Korhogo | 1.41 | 3.50 | 6.80 |
| 18:40 | 2155 | Rustaq Club vs Oman Club | 2.59 | 2.46 | 3.26 |
| 19:00 | 1844 | Doxa Katokopia vs Pafos FC | 6.21 | 3.88 | 1.47 |
| 20:00 | 2478 | Omonia Nicosia vs Apoel Nicosia | 2.42 | 3.17 | 2.70 |
| 20:00 | 4532 | Norway W vs Uruguay W | 1.13 | 6.84 | 14.51 |
| 20:45 | 3499 | FC Winterthur vs Servette Geneva | 2.92 | 3.24 | 2.36 |
| 21:00 | 2840 | EC Agua Santa SP vs Bragantino SP | 3.31 | 3.21 | 2.06 |
| 21:00 | 4122 | Germania Halberstadt vs BSG Chemie Leipzig | 4.88 | 3.95 | 1.56 |
| 21:00 | 4663 | Viktoria Berlin vs Chemnitz | 4.09 | 3.52 | 1.75 |
| 21:30 | 4559 | AC Siena vs Sassari Torres | 2.02 | 3.14 | 3.89 |
| 22:00 | 5616 | Costa Rica W vs Colombia W | 5.59 | 3.99 | 1.49 |
| 22:30 | 1613 | Wales W vs Philippines W | 1.50 | 3.95 | 5.61 |
| 22:30 | 2790 | Juventus U23 vs Foggia | 2.31 | 3.11 | 2.90 |
| 22:30 | 3589 | Arsenal vs Manchester City | 2.80 | 3.24 | 2.42 |
| 22:30 | 5985 | Vicenza vs Virtus Entella | 1.98 | 3.17 | 3.59 |
| 22:45 | 1227 | Motherwell vs St Mirren | 2.47 | 3.14 | 2.84 |
| 22:45 | 1697 | Swansea vs Blackpool | 1.66 | 3.87 | 4.57 |
| 22:45 | 2749 | Swindon Supermarine vs Hartley Wintney | 1.41 | 4.56 | 5.81 |
| 22:45 | 3143 | Bristol City vs Wigan | 1.99 | 3.33 | 3.62 |
| 22:45 | 3862 | Kingstonian vs Hastings United | 2.69 | 3.32 | 2.34 |
| 22:45 | 4698 | Preston vs Luton Town | 2.83 | 3.02 | 2.53 |
| 22:45 | 4953 | Cray Wanderers vs Folkestone Invicta | 1.93 | 3.58 | 3.32 |
| 22:45 | 5131 | Stoke City vs Huddersfield | 1.84 | 3.32 | 4.27 |
| 22:45 | 5845 | Truro City vs Hanwell Town | 1.47 | 4.27 | 5.41 |
| 23:00 | 2097 | West Bromwich vs Blackburn | 1.67 | 3.62 | 4.85 |
| 23:00 | 3469 | Sheffield Utd vs Middlesbrough | 2.03 | 3.38 | 3.43 |
| 23:00 | 4737 | Real Madrid vs Elche | 1.19 | 6.59 | 12.99 |
| 23:00 | 4796 | Borussia Dortmund vs Chelsea | 2.40 | 3.23 | 2.83 |
| 23:00 | 5071 | Brugge vs Benfica | 4.07 | 3.57 | 1.81 |
| 23:10 | 1539 | France W vs Denmark W | 1.25 | 5.35 | 9.06 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



UKURASA 21

Neymar alitaka Kombe la Dunia 2026

# Rais Samia anunua mabao Simba, Yanga CAF

## ●●●Kila bao milioni tano, wenyewe wasema mama utafurahi, kauli yako ni agizo, hivyo...

**Na Adam Fungamwango**

KUELEKEA mechi za raundi ya pili za Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika zitakazochezwa Jumamosi na Jumapili katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ameahidi kununua kwa Sh. milioni tano kila bao litakalofungwa na Simba na Yanga.

Simba inaiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa wakati Yanga ikibeba jukumu hilo kwa upande wa Kombe la Shirikisho Afrika.

Wawakilishi hao wa nchi, wamepoteza mechi zao za awali za hatua ya makundi zikiwa ugenini, ambapo Simba ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Horoya AC nchini Guinea wakati Yanga ikichapwa mabao 2-0 na US Monastir huko Tunisia.

Simba itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi kuikaribisha Raja Casablanca ya Morocco majira ya saa 1:00 usiku wakati muda kama huo Jumapili, Yanga itaikaribisha TP Mazembe ya DR Congo uwanjani hapo.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, akizungumza katika ziara ya wahariri na waandishi wa habari kwenye mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) na semina ya kuwajengea uwezo wanahabari hao namna ya kuripoti habari zinazohusiana na uchukuzi, jijini Dar es Salaam jana, alisema Rais Samia amemwagiza kutangaza kuwa kila goli litakalofungwa na Simba na Yanga atalinunua kwa shilingi milioni tano.

"Rais Samia amenituma niseme kila goli litakalofungwa na Yanga au Simba ametangaza kulinunua kwa Sh. milioni tano, kazi kwenu wachezaji mkifunga magoli mawili mna Sh. miloni 10, lengo lake pamoja na kufunga magoli, timu zetu zinatakiwa kushinda kwenye michuano hii," alisema Msigwa kwenye semina hiyo akitoa taarifa iliyotoka kwa Rais Samia.

Kwa maana hiyo ni kwamba, Simba na Yanga zitapata wingi wa pesa kutokana na idadi ya mabao watakayofunga kwenye mechi hizo.

Baada ya kauli hiyo ya Rais Samia, Klabu ya Yanga katika mtandao wao wa kijamii wa Instagram, ilisema wameipokea kwa mikono miwili ahadi ya hamasa ya rais.

"Tumeipokea hamasa yako Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan kuelekea mchezo wa wetu wa Kombe la Shirikisho dhidi ya TP Mazembe, na Wananchi tunakuahidi, Jumapili mama utafurahi," iliandika klabu hiyo kwenye mtandao wao huo.

Naye Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, akizungumzia ahadi hiyo ya Rais Samia, alisema wameona taarifa kutoka kwa Msemaji Mkuu wa Serikali, Msigwa akitangaza kwamba Rais Mama Samia atanunua kila goli kwa Sh. milioni tano, hivyo wanaichukulia kauli hiyo kama agizo.

"Sisi kama Simba kwanza tumefurahi, tunaichukulia kama ni agizo, mama anatutaka tukafunge magoli. Tumepokea na Jumamosi tunamwahidi kufunga magoli mengi kadri iwezekanavyo. Wachezaji wako tayari kumfurahisha mama na kuwafurahisha Watanzania," alisema.

Ahmed alisema huo ni zaidi ya mchezo wa kawaida ambao mwanadamu amewahi kuona au kufikiria na wao kama Simba wanachotaka ni jambo moja tu, ni ushindi mbele ya Raja Casablanca.

"Rais wa Heshima wa Simba SC, Mohamed 'Mo' Dewji kwa mapenzi yake na Klabu ya Simba na mashabiki wa Simba, alituomba tupunguze viingilio, hivyo mzunguko sasa ni Sh. 3,000, VIP C - Sh. 10,000, VIP B - Sh. 20,000 na VIP A - Sh. 30,000," alisema.



Robertinho

Alisema kwa mujibu wa CAF, mchezo ni saa 1:00 usiku na kwamba awali walithibitisha kucheza saa 10:00 jioni, lakini ratiba ya mwisho iliyotolewa na CAF imeeleza ni saa 1:00 usiku, hivyo wameliandikia shirikisho hilo kuliomba muda wa mchezo uwe saa 10:00 jioni.

"Naomba kuwaambia mashabiki wa Simba tuanze kujiandaa na muda wa

INAENDELEA UK. 23

## Robertinho: Ni ushindi tu J'mosi

**Na Saada Akida**

WAKATI wapinzani wa Simba, Raja Casablanca wakificha siku yao ya kutua nchini, Kocha Mkuu wa wawakilishi hao wa Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Robertinho Oliveira, amesema wako makini katika kuandaa kikosi chao kwa ajili ya kusaka pointi tatu katika mchezo huo wa pili wa hatua ya makundi.

Simba itakuwa nyumbani ikiwakaribisha Raja Casablanca katika michuano hiyo ya kimataifa, mchezo utakaopigwa Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, saa 1:00 usiku.

Akizungumza na gazeti hili baada ya timu hiyo kurejea nchini ikitokea Guinea ambapo ilipoteza mchezo wao wa kwanza kwa kufungwa bao 1-0 dhidi ya Horoya AC, Robertinho alisema leo kikosi kitaingia kambini na kuendelea na mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya mchezo huo ambao wanahitaji pointi tatu katika uwanja wa nyumbani.

Alisema anafurahi kuona wachezaji wake wote wako fiti na kurejea kwa kiungo mshambuliaji wao, Saido Ntibazonkiza ambaye atakuwa msaada mkubwa baada ya kuikosa mechi ya kwanza.

"Tunarejea nyumbani, wachezaji leo watapumzika na kesho (leo) tutaendelea na programu ya mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wetu dhidi ya Raja Casablanca, tuko nyumbani ni faida kubwa kwetu kuutumia vizuri na kupata ushindi.

"Raja Casablanca ni wazuri na wametoka kushinda mechi ya kwanza na sisi tumepoteza ugenini, tulianza maandalizi yetu nchini Guinea na tunaendelea tulipoishia, tutacheza kwa nidhamu na tahadhari kubwa ili kufikia malengo yetu," alisema kocha huyo.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Imani Kajula, alisema kwa upande wao wamekamilisha maandalizi kuelekea mchezo huo wa Jumamosi na leo watazindua kampeni yao kwa kauli mbinu yao kwa kaulimbinu yao ya "Tunawasha Moto" maeneo ya Tegeta, kuelekea mchezo dhidi ya Raja Casablanca.

"Kiutawala mambo yako vizuri

INAENDELEA UK. 23



9 770856 541002 >